Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Saba

## The Sardisean Church Age

Ufunuo 3:1-6

*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye na hizo Roho saba za Mungu, na zile nyota saba. Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa.*

*Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa. Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu Wangu.*

*Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.*

*Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja Nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili.*

*Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, Nami nitalikiri jina lake mbele za Baba Yangu, na mbele ya malaika Zake.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaaambia makanisa.*

**SARDI**

Sardi ulikuwa mji mkuu wa Lidia ya kale. *Ulitoka katika mikono ya wafalme wa Lidia ukawa wa Waajemi halafu ukatekwa na Alekzanda Mkuu.* Ulitekwa na Antioka Mkuu. Ndipo Walfame wa Pergamo wakafaulu kuutawala mpaka wakati Warumi walipouteka. Katika wakati wa Tiberia ulikumbwa na matetemeko ya ardhi na tauni. Siku hizi ni lundo la magofu na haukaliwi na watu.

Mji huu wakati mmoja ulikuwa muhimu sana kibiashara. Plini alisema ya kwamba ustadi wa kutia sufu rangi ulibuniwa hapa. Ulikuwa ni kituo cha kutia sufu rangi na kufuma mazulia. Eneo hili lilikuwa na fedha nyingi na dhahabu nyingi na inasemekana ya kwamba sarafu za dhahabu kwa mara ya kwanza zilitengenezwa hapo. Ulikuwa pia na soko la watumwa.

Dini ya mji huu ilikuwa ibada chafu ya kuabudu mungu wa kike Sibele. Magofu makubwa sana ya hekalu hilo yangali yanaweza kuonekana.

Utakumbuka ya kwamba katika Wakati wa Pergamo nilitaja ya kwamba lile wazo la Kibabeli la "mama na mwana" wanaojulikana kama Semiramisi na Ninusi walikuwa Sibele na Deoiusi wa Asia. Sifa zao hawa wawili zinazoambatana nao zinatoa mwanga sana tunapowachunguza sambamba.

Huyu mwana alikuwa ndiye mungu jua; mama alikuwa mungu mwezi.

Mwana alikuwa bwana wa mbinguni; mama alikuwa malkia wa mbinguni.

Mwana alikuwa mfunuzi wa fadhili na ukweli; mama alikuwa wa upole na rehema.

Mwana alikuwa mpatanishi; mama alikuwa mpatanishi wa kike.

Mwana alikuwa na ufunguo ambao hufungua na kufunga malango ya ulimwengu usioonekana; naye mama alikuwa na ufunguo aina hiyo hiyo akifanya yale yale.

Mwana alikuwa hakimu wa waliokufa; mama alisimama karibu naye.

Mwana alipouawa, alifufuka na kupaa mbinguni; mama alipelekwa kule katika mwili na mwanawe.

Sasa huko Rumi mungu yuyu huyu anapewa sifa za Bwana wetu: yeye anaitwa Mwana wa Mungu wakati mama anaitwa mama wa Mungu.

Sasa jambo hilo ndilo tulililoliona kule nyuma katika nyakati zile nyingine mbili, ambapo wazo la „mama na mwana" lilichukua uhusiano mkubwa sana. Lakini sasa angalia ya kwamba kama vile ilivyokuwa kule nyuma huko Babeli kwamba ibada ya mwana ilianza kuzidiwa na ibada ya mama, kwa hiyo, mama akaanza kupachukua kabisa mahali pa mwana. Tunaona katika wakati huu ya kwamba ibada zote za kipagani za Sardi zilikuwa ibada za kumwabudu mwanamke. Ilikuwa ni Sibele peke yake, si Sibele na Deoiusi. Mama amepachukua mahali pa Mwana kabisa, akijaliwa sifa za Uungu. Mtu anachohitaji kufanya tu ni kupitia katika sifa zake mbalimbali na kukumbuka sifa nzuri sana alizopewa Mariamu na Kanisa la Kirumi kuelewa mahali dini ya wakati huu ilikotoka.

Mambo mawili yalinigusa kwa nguvu nilipochunguza ibada hii ya Sibele. Jambo moja lilikuwa ukweli kwamba alivaa ufunguo kama wa Janusi ambao ulimpa mamlaka yale yale kama ya Janusi, (ufunguo wa mbinguni na duniani na mafumbo ya miungu) na ukweli kwamba waabuduo hujicharaza mijeledi mpaka damu itoke miilini mwao, jambo ambalo linafanywa leo hii na Wakatoliki wanaoona kwamba wanateseka kama Bwana.

Ukweli kwamba huu ndio wakati wa kwanza wa kutengana halisi na Rumi ya papa ambayo ilistawi kweli, bila shaka ilimsababisha nabii wa kike Yezebeli kuimarisha na kutilia mkazo fundisho lake la ibada ya Mariamu katika upinzani wa dhahiri dhidi ya Waprotestanti ambao walimkanushia kuwa na sehemu yo yote katika mpango wa Wokovu achilia mbali kukubalika kwake mbele za Mungu kama bikira aliyechaguliwa kumzaa yule Mwana. Wakati Luther alipokuwa anadhihirisha fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani wao walishikilia matendo, vitubio, maombi na njia nyingine zisizo za kimaandiko. Na wakati Wakristo waliokuwa huru walipomtukuza Mwana, Wakatoliki wa Kirumi walizidisha kumpa Mariamu sifa za kuwa Mungu mpaka karne ya ishirini ikamwona (huku wanatheolojia wa Kirumi walio na vyeo vya juu sana wakipinga) Papa Piusi akimwinua Mariamu dhahiri kabisa atukuzwe katika mwili uliofufuka. Fundisho hilo ni la Kibabeli kabisa la mwana anayembeba mama mbinguni katika mwili.

Si ajabu wakati huu wa tano unaenda moja kwa moja pamoja na nyakati zile nyingine na utaendelea hivyo mpaka utakapoishia katika ziwa la moto ambamo yule kahaba na watoto wake wanauawa katika mauti ya pili. Hilo hapo, ibada ya Mariamu, kumwabudu Sibele. Jambo lingine, je! ulijua kwamba Sibele alikuwa ndiye yule Astarte ambaye Yezebeli alikuwa ndiye kuhani wake wa kike naye aliwafanya Israeli wajikwae kwa ibada zake za kiasherati ambazo aliendesha? Naam, hivyo ndivyo alivyokuwa katika Biblia.

**WAKATI**

Wakati wa Sardi ama wakati wa tano wa lamosa ulidumu kutoka 1520 hadi 1750. Kwa kawaida unaitwa Wakati wa Matengenezo.

**MJUMBE**

Mjumbe wa wakati huu ndiye mjumbe anayejulikana vizuri sana wa nyakati zote. Alikuwa ni Martin Luther. Martin Luther alikuwa ni msomi hodari wa tabia ya upole. Alikuwa akisomea uanasheria wakati ugonjwa uliomsumbua sana na kifo cha rafiki yake msiri vilimfanya ayachunguze sana maisha yake ya kiroho. Aliingia kwenye nyumba ya watawa ya Augustino huko Erfurt mnamo 1505. Hapo alisomea falsafa na pia Neno la Mungu.

Aliishi maisha magumu sana ya kujitesa kwa vitubio lakini matendo yote ya nje hayakuweza kuondolea mbali kujiona yu mwenye dhambi. Alisema, "Nimeijitesa nusura nife kwa madhumuni ya kufanya amani na Mungu, bali nilikuwa gizani wala sikuipata hiyo amani." Mtumishi wa askofu wa shirika lake, Staupizi, alimsaidia kutambua ya kwamba wokovu wake ungepaswa kuwa ni tukio la tendo la ndani wala si ibada za kidini. Alipotiwa moyo hivi, alimtafuta Mungu zaidi. Baadaye akawa padre. Hakuwa ameokolewa hadi wakati huo.

Akawa mwanafunzi mwenye bidii sana na mwenye kina wa Neno na wa masomo ya hali ya juu ya kitheolojia ya siku zake. Alipendwa sana kama mwalimu na mhubiri kwa ajili ya maarifa yake yenye kilindi na unyofu mkuu. Ili kuondoa nadhiri aliyokuwa amejiwekea mwenyewe alienda huko Rumi. Huko aliona upuzi wa matendo ya sheria za kanisa ambazo zilidaiwa kwamba zinaleta wokovu, ndipo Neno la Mungu likawa dhahiri moyoni mwake, "Mwenye haki ataishi kwa imani."

Aliporudi nyumbani ukweli huo wa kiinjilisti wa Andiko hili ukafurika moyoni mwake ndipo akawekwa huru na dhambi na kuzaliwa katika ufalme wa Mungu. Mara baada ya jambo hili alipandishwa cheo akawa Daktari wa Uungu na akaagizwa, "kuyatumia maisha yake yote katika kusoma na kufafanua kwa uaminifu na kutetea Maandiko matakatifu." Akafanya jambo hili, na kwa matokeo makubwa sana hivi kwamba moyo wake na mioyo ya wale waliomzunguka ilielekezwa sana kwenye kweli ya Neno. Mara Neno likaanza kuhitilafiana waziwazi na matumizi mabaya ya kanuni za imani za kanisa pamoja na mafundisho yake.

Hivyo basi wakati Leo X alipotawazwa kuwa papa, na John Tetzel akaja kuuza vitubio vya dhambi, Luther hakuwa na la kufanya ila kusimama dhidi ya fundisho hili lisilo la Kimaandiko. Kwanza, alinguruma kutoka mimbarani dhidi ya jambo hilo halafu akaandika zile hoja zake 95 zinazojulikana sana ambazo tarehe 31 mwezi wa Oktoba mwaka wa 1517 alizigongomea misumari kwenye Mlango wa Kanisa la Castle.

Muda si muda Ujerumani ikawa inawaka moto na matengenezo yalikuwa yamepamba moto. Sasa na ikumbukwe ya kwamba si Martin Luther pekee aliyekuwa amelipinga Kanisa Katoliki la Kirumi. Yeye alikuwa mmoja tu wa wengi. Wengine walikuwa wamewakatalia mapapa mamlaka yao waliyojipa wenyewe ya maisha ya kimwili na ya kiroho, na hata miongoni mwa mapapa kulikuweko na mabadiliko madogo-madogo ya muda. Naam, kulikuweko na wengine wengi waliotoa hoja, lakini katika kisa cha Luther, wakati wa Mungu ulikuwa umeiva kwa kitendo dhahiri ambacho kingekuwa ndio mwanzo wa kurudishwa kwa kanisa kuelekea kwenye kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika wakati wa baadaye kabisa.

Sasa Martin Luther, mwenyewe, alikuwa Mkristo nyeti aliyejazwa na Roho. Hakika alikuwa mtu wa Neno kwa kuwa hakuwa tu na shauku kuu ya kulisoma bali kulifanya lipatikane kwa wote kusudi wote wapate kuishi kwalo. Yeye alitafsiri Agano Jipya na kuwapa watu. Kazi hii ya utumishi aliifanya yeye mwenyewe, akisahihisha kifungu hata mara ishirini. Aliwakusanya wanazuoni wa lugha ya Kiebrania waliomzunguka ambao kati yao walikuwamo Wayahudi na wakafasiri Agano la Kale.

Kazi hii kuu sana ya Luther bado ingali ndiyo kazi ambayo katika hiyo tafsiri zote zilizofuata za Maandiko katika Ujerumani zimetegemea.

Yeye alikuwa mhubiri mwenye uwezo mkuu sana na mwalimu wa Neno, naye akasisitiza hasa sana katika miaka yake ya kwanza ya kujulikana sana na watu, ya kwamba Neno ndilo lililokuwa kipimo pekee. Hivyo basi alipinga kwamba matendo ndio njia ya wokovu na ubatizo kwamba ndio njia ya kuzaliwa mara ya pili. Alifundisha upatanisho wa Kristo mbali na wa mwanadamu kama lilivyokuwa wazo la asili la Penteksote. Alikuwa mtu aliyekuwa anaomba sana na alikuwa amejifunza ya kwamba kadiri alivyokuwa na kazi nyingi zaidi za kufanya, na kadiri alivyokosa wakati kabisa, ndivyo alivyomtolea Mungu wakati wake mwingi katika maombi kusudi ahakikishe anapata matokeo yanayoridhisha. Alijua vile ilivyo kupigana na ibilisi na inasemekana ya kwamba Shetani siku moja alimtokea dhahiri, naye akamtupia kidau cha wino, akimwamuru aondoke. Wakati mwingine washupavu wawili wa dini walimjia kumshawishi ajiunge nao katika kuwaangamiza mapadre wote na kuharibu Biblia zote. Aliitambua roho iliyokuwa ndani yao na akawafukuza.

Imeandikwa kuhusu Dk. Martin Luther katika Historia ya Sauer Chuo cha 3, ukurasa wa 406 ya kwamba yeye alikuwa, "nabii, mwinjilisti, mnenaji kwa lugha, mtafsiri, katika mtu mmoja, aliyejaliwa karama zote tisa za Roho."

Kile kilichouchochea moyo wake kwa Roho Mtakatifu, na ambacho kilikuwa ni shina changa la kijani kibichi ambalo lilionyesha ya kwamba kweli ilikuwa inarudi kanisani kama ilivyojulikana pale Pentekoste, ilikuwa ni fundisho la kuhesabiwa haki: wokovu kwa njia ya imani, mbali na matendo. Ninatambua ya kwamba Dk. Luther hakuamini tu, na kuhubiri tu, kuhesabiwa haki, lakini hilo lilikuwa ndilo lililokuwa jambo lake kuu kama ambavyo kweli ilipaswa kuwa kwa kuwa hilo ndilo fundisho la msingi la ukweli wa Neno. Yeye daima atajulikana kama chombo kile katika mkono wa Mungu ambaye alifufua kweli hii. Alikuwa ndiye mjumbe wa tano na ujumbe wake ulikuwa, "MWENYE HAKI ATAISHI KWA IMANI." Kwa hakika tunakiri ya kwamba yeye alijua na alifundisha ya kwamba tunapaswa twende toka imani hadi imani. Ufahamu wake wa ajabu wa mamlaka, uteule, kuchaguliwa tangu zamani na kweli nyingine zinamwonyesha yeye kuwa mtu mashuhuri sana katika Neno, hata hivyo ninasema tena, kama wasemavyo wanahistoria, Mungu alimtuma kuwaletea watu kipimo cha Mungu dhidi ya matendo_"Mwenye haki ataishi kwa imani."

Sasa kama nilivyosema tayari, wakati huu umeitwa na wanahistoria, Kipindi cha Matengenezo. Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo ulivyokuwa. Ulipaswa kuwa hivyo kwa kuwa Martin Luther alikuwa ni mtengenezaji, si nabii. Sasa najua kitabu cha historia kinamwita nabii, lakini hiyo haimaanishi ya kwamba kitabu hicho cha historia kiko sahihi, kwa maana hakuna taarifa ya Martin Luther kupata sifa ya nabii wa kweli wa Mungu katika maana halisi ya Kimaandiko ya neno hilo. Yeye alikuwa mwalimu mzuri aliyekuwa na baadhi ya madhihirisho ya Roho katika maisha yake nasi tunamsifu Mungu kwa ajili ya jambo hilo. Kwa hiyo hakuweza kuliongoza kanisa liirudie kweli yote kama vile ambavyo angefanya mtu kama mtume Paulo ambaye alikuwa mtume na nabii pia.

Sasa wakati ulipoendelea tunaona badiliko kuu katika njia aliyoendeleza mambo ambayo alihusika nayo. Hapo mwanzoni alikuwa mpole sana, mjasiri sana, mwenye subira sana na daima alimngojea Mungu kuzitatua shida. Lakini baadaye watu wengi wakaanza kuja chini ya bendera yake. Kusudi lao halikuwa kweli la kiroho. Sana sana walikuwa na msukumo wa kisiasa. Walitaka kuvunja nira ya papa. Hawakupenda kutuma pesa Rumi. Washupavu wa dini wakainuka. Mara alikokotwa akaingizwa katika mambo ya siasa na maamuzi ambayo kwa kweli yalikuwa nje ya mambo ya kanisa ila kwamba kanisa kwa njia ya maombi, kuhubiri na mwenendo huenda likaweka kielelezo cha kufuatwa. Matatizo haya ya kisiasa yaliongezeka mpaka akaingizwa kwa nguvu katika mahali pabaya pa kuwapatanisha matajiri na maskini. Maamuzi yake yalikuwa mabaya sana hivi kwamba maasi yalitokea na maelfu wakauawa. Yeye alikusudia mema, lakini mara alipokwisha kujifunga tena katika Injili ya muungano wa Kanisa na Serikali ilibidi avune kimbuga.

Lakini kwa hayo yote, Mungu alimtumia Martin Luther. Hebu na isisemwe ya kwamba makusudi yake yalikuwa ni mabaya. Na isemwe tu kwamba uamuzi wake ulishindwa. Kweli kama Waluteri wangalirudi kwenye mafundisho yake na kumtumikia Mungu kama ndugu huyu mwenye neema alivyomtumikia Yeye, basi hao watu hakika wangekuwa heshima kubwa na sifa kwa Mungu aliye mkuu na Mwokozi, Yesu Kristo.

**SALAMU**

Ufunuo 3:1,

*"Haya ndiyo anenayo Yeye Aliye na hizo Roho saba za Mungu, na zile nyota saba."*

Mara nyingine tena kama vile katika zile nyakati nne zilizopita Roho anatufunulia Bwana wetu wa neema kwa kueleza sifa zake za ajabu. Wakati huu Yeye akiwa amesimama katikati ya kanisa, tunamwona Yeye kama Yule aliye na zile Roho saba za Mungu na zile nyota saba. Tunajua zile nyota saba ni akina nani, lakini itatubidi kujua zile Roho saba ni kitu gani.

Kifungu hiki cha maneno kinapatikana mara nne katika Kitabu cha Ufunuo.

Ufunuo 1:4,

*"Na zitokazo kwa Roho saba Walioko mbele ya kiti Chake cha enzi."*

Ufunuo 3:1,

*"Haya ndiyo anenayo Yeye Aliye na hizo Roho saba."*

Ufunuo 4:5,

*"Na katika kile kiti cha enzi kunatoka umeme na sauti na ngurumo. Na taa saba za moto zilikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi, ndizo Roho saba za Mungu."*

Ufunuo 5:6,

*"Nikaona, na tazama, katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote."*

Kwanza, tunajua bila shaka kwamba aya hizi hazifundishi fundisho jipya na kinyume na Yohana 4:24a "Mungu ni Roho (mmoja)." Lakini hii ni kama I Wakorintho 12:8-11 ambamo tunaona Roho Mmoja akijidhihirisha Mwenyewe katika njia TISA. Kwa hiyo tunajua ya kwamba zile Roho Saba za Mungu zinamaanisha ni Roho yule yule mmoja akija kwa namna ya njia saba. Sasa katika Ufu. 4:5 Roho zizi hizi saba zinaitwa „taa za moto zikiwaka" mbele za Bwana. Kwa kuwa Yohana hakutumia kitu ila mifano ya Agano la Kale katika Ufunuo tunaenda kwenye Agano la Kale na kuona kutoka katika Mit. 20:27 ya kwamba "Pumzi ya mwanadamu ni taa ya Bwana." Hizi Roho saba zinaonekana zina uhusiano na mwanadamu. Yohana Mbatizaji katika Yohana 5:35 aliitwa „nuru iwakayo" ambayo kweli ingepaswa kutafsiriwa kama „taa iwakayo". Tena katika Ufu. 5:6 zile Roho saba zinatambulishwa kama macho saba.

Katika Zekaria 4:10,

*"Maana ni nani aliyeidharau siku ya mambo madogo? kwa kuwa watafurahi, nao wataiona timazi katika mkono wa Zerubabeli; naam, hizi saba ndizo macho ya Bwana."*

Ni dhahiri sana kwamba neno, 'wao' linamaanisha watu. Hivyo tunaona ya kwamba macho ya Bwana katika mfano huu ni watu_bila shaka watakuwa ni watu waliotiwa mafuta, wamejaa Roho Mtakatifu, kwa maana huduma za Mungu haziko chini ya mamlaka ya wanadamu bali ya Roho Mtakatifu. Tukiuweka uvumbuzi wetu wa Maandiko pamoja ni dhahiri ya kwamba hizi Roho saba za Mungu zinahusu huduma inayoendelea ya Roho Mtakatifu yule yule katika maisha ya watu saba ambao Mungu anajitambulisha nao vizuri sana. Hao ndio macho Yake, nao ndio taa Zake. Kwamba watu hawa saba ni akina nani inaweza kuonekana kwa urahisi kwa sababu katika fungu la maneno linalofuata linawaita zile nyota saba ambazo tayari zinajulikana kwetu kama wale wajumbe saba wa zile nyakati saba. Jinsi hilo lilivyo zuri. Mnaona, nyota hiyo ilikusudiwa kurudisha nuru usiku, kwa maana jua limeshuka. Vivyo hivyo mjumbe (aliyefananishwa na nyota) kwa kila wakati alikusudiwa kurudisha nuru ya Mwana. Wote walifanya jambo hili kwa Roho Mtakatifu.

Paulo alikuwa mjumbe wa kwanza naye alisema katika Gal. 1:8 ya kwamba kama malaika ye yote, mjumbe ye yote, padre ye yote, haidhuru yeye alikuwa ni nani_kama atahubiri injili nyingine yo yote isipokuwa ile aliyohubiri Paulo, na alaaniwe. Paulo alijua ya kwamba baada ya kuondoka kwake, mbwa mwitu wakali wangeingia. Alijua ya kwamba Shetani, mwenyewe, angeweza kutokea kama malaika wa nuru kwa hiyo ni zaidi sana vipi watumishi wake. Kwa hiyo anaonya ya kwamba Injili hii daima ingekuwa ni ile ile. Sasa Paulo alikuwa amebatiza katika Jina la Yesu na akabatiza tena ambapo watu hawakuwa wamezamishwa wakabatizwa majini kwa jinsi hiyo. Aliliweka kanisa katika utaratibu na akafundisha matumizi halisi ya karama za Roho na kuthibitisha ya kwamba zilipaswa kubaki kanisani mpaka Yesu atakapokuja. Hivyo basi wajumbe waliofuatia, hao wote sita waliosalia, kwa moto uo huo wa Roho Mtakatifu, wangewaka na kutoa nuru ile ile ya Injili ya Yesu Kristo na ishara zingewafuata wao. Je, Ireneo alistahili? Naam. Je! Martin? Naam. Je, Columba? Naam. Je! Martin Luther? Hakika kabisa. Je! Wesley Naam bwana, alikuwa na huduma kuu na hata akamwombea farasi wake apate afya na akapona. Haya basi. Nyakati saba za kanisa na wajumbe saba waliokuwa wa namna moja, naye Paulo akatangaza laana kwa ye yote aliyesema alikuwa ni mjumbe lakini alikuwa na injili tofauti na aliishi katika nuru tofauti.

Je! hilo tamshi langu la mwisho linaafikiana na Neno jingine lote? Naam. Inasemwa katika Neno ya kwamba kama mtu ye yote akiongezea kwenye kitabu hiki ama akiondoa kwake, atapigwa kwa mapigo na kuhukumiwa aende hukumuni na Mungu.

Mungu alisema,

> *"Nitamwongezea mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki ama nitaondoa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima."*

Ufunuo 22:18.

Kwa hiyo tunaona ya kwamba zile Roho Saba kweli zinamtaja yule Roho Mmoja wa Mungu akitenda mapenzi ya Mungu na kutekeleza Neno Lake katika vizazi mbali-mbali. Ningetaka kutoa mfano wa jambo hilo kutoka kwenye Neno. Roho wa Mungu alikuwa juu ya Eliya akitenda kazi kwa nguvu sana. Halafu Roho yuyo huyo akaja juu ya Elisha katika nguvu maradufu. Halafu karne kadha baadaye, Roho yule yule tunayemwita Roho wa Eliya ili kuelezea huduma Yake, akarudi juu ya Yohana Mbatizaji. Siku moja Roho yuyo huyo akitambulishwa kwa huduma ya namna hiyo hiyo atakuja juu ya mtu fulani kwa ajili ya mwisho wa wakati wa kanisa la Mataifa.

Tena: Maandiko yanasema ya kwamba Mungu alimtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na nguvu Naye akazunguka huko na huko akitenda mema, akiponya wote walioonewa na ibilisi. Wakati Yesu alipokuwa anaondoka aliwaambia wanafunzi Wake wangoje mpaka Pentekoste wakati ambapo Roho yule yule aliyekuwa juu Yake angerudi na kushuka juu yao na kuwajaza. Ndipo „mwili huo ulioitwa" (kanisa) ungekuwa badala Yake juu ya nchi, ukipachukua mahali pake. Na kwa sababu Roho yule yule Ambaye alikuwa ndani Yake angekuwa ndani yao, wangefanya kazi zile zile. Na watu wo wote ambao kweli ndio Mwili wa Yesu Kristo (kanisa la kweli) watadhihirisha kazi zile zile kama alizozifanya Yesu na kanisa la Pentekoste kwa sababu Roho yule yule atakuwa ndani yao. Kanisa lingine lo lote lisilokuwa na Roho na madhihirisho litatoa hesabu yake kwa Mungu.

Inanenwa hapa pia ya kwamba nyota hizi saba, ama wajumbe saba kwa zile nyakati saba wako katika mkono Wake. Yeye anawashikilia. Unajua mara moja ya kwamba kama zimeshikwa katika mkono Wake wanahusiana na nguvu Zake. Hilo ndilo mkono unaloomaniisha. Unamaanisha nguvu za Mungu! Na mamlaka ya Mungu. Hakuna hata mmoja wao aliyekuja katika nguvu zake mwenyewe na mamlaka. Hivyo ndivyo Paulo alivyosema. Hakuna mtu angalithubutu. Inahitaji mamlaka ya Mungu na nguvu za Roho Mtakatifu. Injili inahubiriwa na mamlaka ya Mungu katika nguvu za Roho. Watu hawa wote walipewa nguvu na Roho Mtakatifu. Wote waliukabili ulimwengu. Wangeweza kufanya hivyo. Walikuwa wamejaa Mungu. WALITUMWA ama waliamriwa na Mungu WALA si wenyewe ama watu wengine.

Sasa walikuwa na kile ulimwengu usingeweza kuwa nacho. Yesu alisema ya kwamba wakati alipoondoka angemtuma Roho Wake Ambaye ulimwengu haungeweza kumpokea. Hiyo ni kweli. Ulimwengu, ama mifumo ya ulimwengu haingeweza kumpokea. Hivyo ndivyo madhehebu yalivyo—ni mfumo wa ulimwengu. Nionyeshe kanisa la mfumo wa ulimwengu lililojaa Roho Mtakatifu. Ninataka kuliona. Kama unaweza kunionyesha kanisa kama hilo unaona kosa katika Neno. La bwana. Hakuna hata mmoja wa wajumbe hawa aliyekuwa ameunda dhehebu. Aidha walitolewa nje ama walitoka kwa sababu walihakikishwa juu ya dhambi ya madhehebu. Roho Mtakatifu anawezaje kuwa kwenye madhehebu wakati madhehebu ndiyo yanayopachukua mahali pa Roho pia madhehebu yanapachukua mahali pa Neno? Kumbuka, "Madhehebu" ni "MAUTI". Haiwezi kuwa njia nyingine yo yote. Kama ulimwengu ukichukua mamlaka, Roho anaondoka.

Naam, Roho si Roho saba bali ni MMOJA. Yeye daima atakuwa yeye yule na kutenda vile vile. Na hao wajumbe saba watakuwa na Roho yule yule na kufundisha Neno lile lile na kuwa na nguvu zile zile. Na kama kanisa hilo ni kanisa la kweli litakuwa na Roho yule yule na Neno na matendo ya nguvu waliyokuwa nayo ule wakati wa Pentekoste. Kwa ujuzi litakuwa kanisa la Kipentekoste; na kutakuweko na lugha, na tafsiri na unabii na kuponya. Mungu atakuwa katikati yake na Mungu atajitangaza Mwenyewe katikati yake kama vile alivyofanya daima. Haleluya! Naye atakuwa asiye na utaratibu. Usisahau jambo hilo.

Sasa tunaweza kuona ya kwamba Yesu Kristo anajifunua Mwenyewe katika nyakati zote kwa Roho Wake katika wale wajumbe. Wao ni kama Musa alivyokuwa kwa wana wa Israeli. Kama alivyokuwa na ufunuo kwa ajili ya siku yake, vivyo hivyo kila mjumbe alikuwa na ufunuo wa Mungu na huduma kwa siku hiyo.

Kwa hivyo tunapoona ya kwamba wajumbe wako mkononi Mwake, tunaona Bwana akijitambulisha Mwenyewe pamoja na watu hawa na kuwapa nguvu Zake. Haitoshi kwamba Yeye amejihusisha na kanisa zima, jambo ambalo tuliliona wakati alipoonekana amesimama miongoni mwa vinara vya taa saba vya dhahabu. Wala hata haitoshi ya kwamba tunaziona zile huduma tano za Waefeso nne (mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji). Kwa kuwa katika kila wakati kanisa hupotoka, wala si wafuasi tu bali na kundi la makasisi_wachungaji wako makosani na kondoo pia. Ndipo Mungu anajitokeza jukwaani kama Mchungaji Mkuu katika huduma za hawa watu saba kuwaongoza watu Wake wairudie ile kweli na zile

nguvu nyingi za kweli hiyo.

Mungu yuko ndani ya watu Wake_watu Wake wote, kwa maana kama mtu ye yote hana Roho wa Kristo yeye si Wake. Naye ni Neno. Hilo lingekuwa ni Neno linalotambuliwa katika watu. Lakini Yeye ameweka uongozi maalum katika watu hawa aliowachagua na kwa shauri la mapenzi Yake. Wanaonekana mara moja katika kila wakati. Ni Roho yule yule ndani yao. Ni kilio cha mbali jinsi gani na huu uzushi wa Rumi. Wana mtu waliyemchagua wenyewe_mmoja baada ya mwingine_hakuna hata mmoja anayeonyesha nguvu za Mungu_hakuna hata mmoja anayedumu katika Neno la Mungu_kila mmoja akihitilafiana na yule aliyemtangulia na kuongeza yale anayotaka kana kwamba alikuwa Mungu. Mungu hayumo ndani yake. Lakini Yeye yuko ndani ya mjumbe Wake na yeye ambaye angekuwa na utimilifu wa Mungu angemfuata huyo mjumbe kama vile huyo mjumbe alivyo mfuasi wa Bwana kwa Neno Lake.

*"Yeye aliye na hizo Roho saba za Mungu na zile nyota saba."*

Ufunuo 3:1.

Kama vile Bwana yuyu huyu anavyojitambulisha Mwenyewe na mwanadamu katika kule kufanyika mwili, Yeye tena anajitambulisha Mwenyewe na mwanadamu kwa Roho Wake ndani ya mwanadamu. "Hawa ni Wangu," asema Bwana. Hao wajumbe saba waliojazwa na Roho ni wa Bwana. Wanaweza kukataliwa. Wanaweza kuhojiwa. Naam, kwa akili za wanadamu huenda hata wasionekane kwamba wanastahili_hata hivyo, wao ni wajumbe kwa wakati wao. Mungu alimtumia Ibrahimu (akasema uongo), akamtumia Musa (akaasi), Yona (akakaidi), Samson (akafanya dhambi), Daudi (akaua). Pia alimtumia Yoshua, na Yusufu. Na hao walio na hitilafu mbaya sana ni wengi sana kuliko hao ambao historia zao zinaonekana kuwa kamilifu. WOTE WALIKUWA, NA WANGALI NI WAKE. Hakuna anayeweza kuthubu kukanusha hilo. Aliwatumia kupitia na kwa njia ya Roho Mtakatifu aliyemweka ndani yao. Walisimama ama kuanguka mbele za Bwana wao wenyewe. Na ndani yao hao wote yalitimizwa mapenzi ya mamlaka ya Mungu. Acha historia ya nje ijaribu kukanusha jambo hili, lingali linasimama. Yule Mungu wa milele angali anatembea katikati ya vinara vya taa vya dhahabu na huwatuma wajumbe Wake kwa Roho Wake wakiwa na lile Neno kwa watu wa kila wakati.

**SHTAKA**

Ufunuo 3:1b,

> *"Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa."*

Ufunuo 3:2b,

> *"Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu."*

Sasa hapa, hakika, ni jambo la ajabu sana. Katika kila wakati mpaka sasa Roho kabla ya yote amewasifu waamini wa kweli, halafu akaulaumu mzabibu wa uongo. Lakini katika kipindi hiki inaonekana kuna upotovu mwingi sana wa kumdharau Mungu na Neno Lake hivi kwamba ujumbe wote wa wakati huu wa tano unanguruma hukumu.

*"Nayajua matendo yako."*

Ni matendo gani haya yaliyokuja mbele za Bwana na kusababisha Yeye kuudhika? Vema, unajua ya kwamba kila wakati ulipita ukaingia kwenye ule uliofuata, kwa hiyo tuna kuendelea kwa kazi za wakati wa nne kuingia katika ule wa tano. Matendo haya kama mnavyoyafahamu vizuri sana yalikuwa:

Uongozi wa Roho Mtakatifu ulibadilishwa na uongozi wa wanadamu.

Neno safi la Mungu na fadhili zake zinazotolewa bure kwa watu wote lilibadilishwa kwa kanuni za imani, mafundisho ya sharti, amri za kanisa, nk.

Kule kuabudu katika Roho na Karama za Roho na yote yale yanayohusu ushirika wa kweli wa kusanyiko la watakatifu yaliondolewa na badala yake zikaingizwa liturgia na ibada halisi za sanamu, karamu za wapagani, nk.

Ibada za kumwabudu Mariamu zilikuwa zikishikilia nafasi kubwa katika ibada za Kikristo, mpaka kwa uhalisi yeye akachukua nafasi ya Uungu na Mwana alishushwa kutoka mahali Pake pa juu kuliko wote akawa chini ya mwanadamu anayeitwa papa, ambaye alijiita aliye mahali pa Kristo.

Wale waliopiga vita kanisa hili baya sana la mpinga-Kristo waliangamizwa. Wale waliodumu nalo walijikuta ni vibaraka vya kanisa haidhuru walikuwa maskini ama wafalme. Maisha yao hayakuwa yao tena, na wala maisha yao hayakuwa ya Kristo, lakini walikuwa mali ya Kanisa la Kirumi mwili, nafsi, na roho. Walizungumza juu ya damu ya Kristo, hata hivyo walinunua wokovu wao kwa pesa, na kununua msamaha wa dhambi kwa aidha dhahabu ama vitubio. Matajiri kati yao walifurahia hali hiyo wakati Papa Leo X alipowaruhusu kununua msamaha wa dhambi ambazo walikuwa bado hawazijatenda kusudi waweze

kupangilia dhambi zao za kutisha kwa dhamira tulivu na halafu waendelee kuzitekeleza, wakijua ya kwamba papa tayari alikwisha kuwasamehe dhambi zao. Neno la Mungu lilifichwa kwao, kwa hiyo ni nani angalijua kweli! Kwa kuwa kweli hutokana tu na Neno, hao watu walifungiwa kwenye korokoro la Kanisa la Kirumi, wakingojea kifo, na baada ya kifo hukumu. Lakini yule kahaba mkuu, aliyelewa kwa damu ya mashahidi na akiwa hana wazo la kuhukumiwa, aliendelea kupepesuka kikatili kuwaua watu kwa mauti ya kiroho na ya kimwili.

Sasa karibu na mwisho wa wakati wa nne ambao ungekuwa mwanzo wa wakati wa tano pia, kuvamiwa kwa Konstantinopo na Waturuki kuliwapeleka Magharibi wanachuoni wa Mashariki na vitabu vyao vya Kiyunani. Hivyo basi usafi wa Neno na mafundisho ya waamini wa kweli vilienezwa. Na si kwamba tu hawa waalimu bora walikuwa muhimu sana lakini pia uvumbuzi wa kile kilichopata kuwa msingi wa mitambo yetu ya kisasa ya kupiga chapa uligunduliwa, ikirahisisha kuchapishwa kwa vitabu. Hivyo basi tunaona ile njaa kubwa na shauku ya Biblia ingejibiwa.

Mungu aliwainua watu wengi hodari ambao Luther alikuwa ni mmoja wao. Kalvini na Zwingli walikuwa ni watu wengine wawili maarufu na mbali na hawa walikuweko na wengine wengi, wengi mno ambao hawajulikani vizuri sana. Hata hivyo, ingawa hayo yote hayakuwa bure, kazi kuu ya Mungu kwa kweli ilizuiliwa na watu hawa hawa. Kwanza, wao HAWAKUPINGA kuungana kwa Serikali na Kanisa kulikofanywa na Baraza la Nikea lakini wao kweli waliunga muungano huo mkono.

Jambo la Injili kutetewa na serikali lilipendwa ingawa hapakuwepo na Neno lililokubaliana na jambo hilo. Na ingawa tunaweza kuona "hasira ya mwanadamu ikimsifu Mungu," katika matukio kama lile la Henry wa Nane akiunga mkono matengenezo na kukataa utawala wa papa, lilikuwa jambo lililokuwa mbali sana na ile kweli ya Pentekoste na ulinzi wa Mungu mwenye nguvu zote.

Ijapokuwa Luther alishikilia kufundisha dhidi ya kuingiliwa kwa mambo ya kanisa la mtaa kutoka nje, hakuweza kuondoa wazo la serikali ya kanisa la "Askofu, Askofu Mkuu" kutoka kwenye mioyo ya watu. Kwa hiyo kanisa lilichukua hatua moja katika mwelekeo wa kweli lakini bado lilibaki limefungwa pingu, kwa hiyo kwa kifupi lilikuwa limefungwa tena katika gereza lile lile lililojaribu kutoroka.

Hata hivyo kile kikombe cha matendo hayo ya kuchukiza hakikuwa kimejaa bado. Si kwamba tu Luther kwa maamuzi mabaya alichochea vita na hivyo basi akasababisha vifo vya umati wa watu; lakini kikundi cha Zwingli kilimtesa mpaka kikampeleka gerezani yule mtawa Dk. Hubmeyer, na ingawa hakikumchoma moto, kwa kweli kilihusika kwa kiwango kikubwa katika kifo chake cha baadaye kwa kuchomwa moto. Na Kalvin naye alikuwemo, kwa kuwa alidai kukamatwa kwa Servetus ambaye alikuwa ameona na kufundisha umoja wa Uungu. Basi serikali ikamhukumu ndugu huyu, naye Kalvin kwa hofu akashtukia wamemchoma moto.

Kama kuliwahi kuweko na wakati wa shauku za umadhehebu ilikuwa ni wakati huu wa huzuni. Maneno ya Komeniasi yanakifafanua kipindi hiki. Komeniasi aliandika „KINATAKIWA KITU KIMOJA". Yeye anaulinganisha ulimwengu na mahali penye mazingile mwanambije, na anaonyesha ya kwamba njia ya kutokea ni kuacha kile ambacho hakihitajiki, na kuchagua kile kitu kimoja kinachotakiwa_Kristo. Wingi wa waalimu, anasema ndiyo sababu ya wingi wa madhehebu, ambayo punde si punde tutaishiwa na majina ya kuyaita. Kila kanisa hujihesabu kuwa ndilo la kweli, au ngaa ndilo sehemu ambayo ndiyo safi kuliko yote na ndiyo sehemu ya kweli, na huku kati yao yanatesana yenyewe kwa yenyewe kwa chuki mbaya sana. Hakuna mapatano yanayoweza kutumainiwa kati yao; wanaukabili uadui kwa uadui usioweza kupatanishwa.

Kutoka kwenye Biblia wanabuni kanuni zao mbalimbali za imani; hizi ndizo ngome zao na maboma yao ambamo wanajilinda na kujibu mashambulizi yote. Sitasema ya kwamba maungamo haya ya imani_kwa sababu tunaweza kukubali mara nyingi ya kwamba ndivyo yalivyo_yenyewe ni mabaya. Yanakuwa mabaya, hata hivyo, kwa sababu yanachochea moto wa uadui; ni kwa kuyatupilia mbali kabisa ndipo ingewezekana kuanza kazi ya kutibu majeraha ya Kanisa. "Katika utata huu wa wingi wa madhehebu na imani mbali mbali kuna jambo jingine: kupenda mabishano .... Faida gani inayopatikana kwake? Je! kuna ubishi hata mmoja wa kielimu uliopata kutatuliwa? Kamwe. Idadi yao imeongezeka tu.

Shetani ndiye mdanganyifu mkubwa kuliko wote; hajapata kushindwa kamwe katika ugomvi wa maneno ... Katika kutumikia Mungu maneno ya wanadamu kwa kawaida husikiwa zaidi ya Neno la Mungu. Kila mmoja hupayukapayuka atakavyo, ama hupoteza wakati katika ubishi wa kielimu wa maneno mengi na kukanusha maoni ya wengine. Kuhusu kuzaliwa upya na jinsi mtu anavyopaswa kubadilishwa na kufanywa mfano wa Kristo kusudi awe mshirika wa Tabia ya Uungu (2 Pet. 1:4), huwa ni shida sana jambo hilo kuongelewa. Kuhusu nguvu za ufunguo, Kanisa karibu limepoteza nguvu za kufunga, ila tu zinabaki nguvu za kufungua ... Zile sakramenti, zilizotolewa kama mifano ya umoja, upendo, na za maisha yetu katika Kristo, zimefanywa kisa cha ugomvi ulio mbaya sana, chanzo cha chuki ya mmoja kwa mwingine, kituo cha umadhehebu ...

Kwa kifupi, Ukristo umekuwa njia zisizoeleweka ambazo hutaweza kujua njia. Imani imegawanyika katika visehemu vidogo-vidogo elfu moja nawe unafanywa mzushi kama kuna kimoja cha hivyo

usichokikubali ... Ni nini kinachoweza kusaidia? Kuna jambo moja tu linalotakiwa, kurudi kwa Kristo, kumtazama Kristo kama Kiongozi wa pekee, na kutembea katika nyayo Zake, kuwekea kando njia nyingine zote mpaka sote tutakapoifikia ile mede, na tutakapoufikia umoja wa imani (Efe. 4:13). Kama vile Bwana wa mbinguni alivyojenga kila kitu kwenye msingi wa Maandiko vivyo hivyo sisi nasi tunapaswa kuacha ubinafsi wetu wote wa imani zetu maalum na kutosheka na Neno la Mungu lililofunuliwa ambalo ni letu sote. Tukiwa na Biblia mkononi mwetu tunapaswa kupaza sauti: ninaamini yale ambayo Mungu amefunua katika Kitabu hiki; nitashika amri Zake kwa utiifu; ninatumainia kile Yeye alichoahidi. Enyi Wakristo, sikilizeni! Kuna uhai mmoja tu, lakini Mauti inatujia sisi katika namna elfu moja. Kuna Kristo mmoja tu, ila Wapinga Kristo elfu moja … Kwa hiyo mnajua, Enyi jamii ya Wakristo wote, jambo moja linalotakiwa. Ama unamrudia Kristo ama unaangamia kama mpinga-Kristo. Kama ninyi ni wenye hekima nanyi mtaishi, mfuateni Kiongozi wa Uzima.

Lakini ninyi, Wakristo, furahini katika kunyakuliwa kwenu,...yasikilizeni maneno ya Kiongozi wenu wa Mbinguni, 'Njoni Kwangu'... Jibuni kwa sauti moja, 'Naam, tunakuja'".

Sasa hivi tu nilisema ya kwamba wakati huu ulisababisha kukua kunakotisha kwa roho ya kimadhehebu. Kama tabia ile ya Wakorintho ya "Mimi ni wa Paulo, mimi ni wa Kefa" ilipata kuonyeshwa, ilikuwa ni wakati huu. Kulikuwa na kundi la Waluteri, Wahusiti, la Wazwingli, nk. Kuvunjika vipande vipande kama huko kwa huo mwili kulikuwa kunasikitisha sana. Walikuwa wakiishi jina bali walikuwa wamekufa. Hakika walikuwa wamekufa. Walikufa dakika ile waliyounda madhehebu. Yale makundi makubwa yaliunda madhehebu na kufunga ndoa na serikali. Hilo lilimaliza kila kitu. Walikuwa wamekwisha. Hawa hapa wale Walutheri waliokuwa wamelikosoa Kanisa Katoliki la Kirumi. Walijua maovu ya miungano ya kisiasa na kiroho_hata hivyo Luther (kama wakati ule Petro alipozidiwa na wale wa Dini ya Kiyahudi) aliendа moja kwa moja na kuifanya serikali badala ya Mungu, kuwa iwe ndiyo mtetezi wa imani. Haya ndiyo madhehebu ya kwanza yenye sifa yaliyotoka kwa yule kahaba, lakini wakati Luther alipokufa hawakuchukua muda mrefu kuwa na serikali ya kidini kama ile waliyokuwa wameipinga. Jambo hili la Mungu, hata kufikia wakati wa kuja kwa kizazi cha pili yalikuwa yamerudi moja kwa moja chini ya ubawa wa mama yake. Yalikuwa yamerudi na hata hayakujua. Walikuwa wamechukua jina lao juu ya Jina Lake. Walikuwa wakiishi majina yao wenyewe, pia.

Na madhehebu yote yanafanya jambo lile lile siku hizi. Wanaishi jina lao wenyewe, wala si Jina la Bwana Yesu Kristo. Hilo linaonekana kwa urahisi kwa kuwa kila kanisa linajulikana kwa jinsi linavyoabudu lakini hakuna linalojulikana kwa nguvu za Mungu. Hilo hapo jaribio lako. Nami nakutaka uone papa hapa ya kwamba kipindi hiki hakikuwa na ishara na maajabu miongoni mwao. Waliacha nguvu za Mungu wakachukua nguvu za serikali. Waling"ang"ania jina lao wenyewe; walijipatia sifa. Ilikuwa ni roho yule wa kale wa kumwingiza kila mtu katika kundi lake. Leo Wabatisti wanawataka Wamethodisti waje kwa Wabatisti. Wamethodisti wamekazana kuwaongoa Wapresbiteri. Wapentekoste wanawataka wote. Kila moja linadai kutoa mengi kuliko yote na kuonyesha matumaini makuu kuliko yote_kitu kama mlango wa kuingilia mbinguni, ama angaa, njia ya nzuri zaidi ya kuingia. Hayo yote yanahuzunisha jinsi gani.

Roho hii ya kimadhehebu imeyafanya madhehebu yote kuandika vitabu vyao vya mafundisho na kufundisha kanuni zao, kuanzisha ofisi zao na serikali za kanisa na kila moja linadai kuwa ndilo, na ndilo pekee, ambalo kweli linanena kwa ajili ya Mungu kwani ndilo linalostahili kuliko mengine yote. Naam, kama hivyo sivyo hasa papa na Kanisa la Kirumi wanavyofanya! Wako wamerudi kule kule wakiwa pamoja na mama yao, yule kahaba, wala hawajui.

Katika kufunga mafafanuzi yetu juu ya aya hii, "una jina la kuwa hai, nawe umekufa," siwezi kuwasisitizia sana ya kwamba wakati huu, ingawa ulileta yale matengenezo, ulikemewa sana na Mungu badala ya kusifiwa, kwa maana ULIPANDA MBEGU ZA MADHEHEBU AMBAYO YALIRUDI MOJA KWA MOJA KWA YULE KAHABA, baada ya Mungu kufungua mlango wa kutokea. Wakati hatua ya kutoka kwenye Kanisa Katoliki ilipotokea, haikuwa kwa kweli ni ya Kiroho kwa jumla, bali zaidi sana ilikuwa ni ya kisiasa. Karibu watu wote waliungana na Uprotestanti kwa sababu, kama nilivyokwisha kusema, walichukia utaratibu wa Kirumi wa utumwa wa kisiasa na wa kiuchumi. Kwa hiyo, badala ya jambo hili kuwa hatua muhimu ya Kiroho yenye dalili zote za ushawishi wa Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa wakati Mungu alipotumia mambo halisi ya Kiroho kutimiza makusudi Yake Pale Pentekoste, ilikuwa kwa kweli ni MATENDO AMBAPO HASIRA YA MWANADAMU ILIMSIFU MUNGU, na matokeo yake yalifanana na ya historia ya Israeli wakati walipoondoka Misri na kuzungukazunguka jangwani, wakashindwa kufika kwenye Nchi ya Kanaani. Hata hivyo, mengi yalitimizwa kwa kuwa mahali ambapo nira hiyo ya Rumi ilivunjwa ngaa kwa sehemu, watu waliweza sasa kupokea Neno la Mungu na kukubali uongozi wa Roho bila ya kuwa na hofu kubwa sana kama ilivyokuwa hapo mwanzoni. Jambo hili lilifungua mlango kwa ajili ya ule wakati mkuu wa kimishenari uliofuata.

Yule Yezebeli wa Thiatira hakuwa na moyo wa kuachilia utawala wake juu ya watu, na hivyo basi tunaona binti yake Athalia akiinua kichwa chake katika Wakati wa Sardi akiwa na matumaini ya kwamba angeweza kuunyonga na kuuua ule mzao wa kweli kwa njama zake za kimadhehebu.

**ONYO**

Ufunuo 3:2,

*"Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu."*

Laiti ingaliwezekana kusemwa kwamba Wakati wa Sardi ungalikuwa wa kurudishwa badala ya kuwa wa matengenezo. Siwezi kusema jambo hilo. Neno haliuiti kurudishwa, bali bila shaka linauita matengenezo. Kama ungalikuwa wa kurudishwa, wakati huo ungekuwa wakati mwingine wa Kipentekoste. Lakini haukuwa ni wakati wa kurudishwa. Sana sana jambo ambalo lingaliweza kusemwa juu yake lilikuwa, *"Ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa."* Kulikuweko na kitu kinachokosekana. Jamani, naam, hakika kilikuwepo. Wakati huu ulikuwa na kuhesabiwa haki, lakini ulikosa kuwa na kutakaswa na Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huo ndio uliokuwa mpango wa kwanza wa Mungu. Hayo ndiyo waliyokuwa nayo wakati wa Pentekoste. Walihesabiwa haki, walitakaswa, na walijazwa na Roho Mtakatifu. Loo! nisikilizeni, sababu ya kuhesabiwa haki na kutakaswa ni kusudi upate kubatizwa na Roho Mtakatifu.

Hiyo ndiyo sababu kuna kanisa. Ni hekalu la Mungu lililojawa na Mungu, yaani Roho Mtakatifu. Roho yule yule aliyekuwa katika Yesu wakati alipokuwa hapa duniani, akimfanya afanye mambo makuu aliyotenda alirudi kwenye kanisa wakati wa Pentekoste hivi kwamba walifanya kazi zile alizozifanya Yeye. Wakati huu haukuwa na kazi hizo. Loo! walikuwa na Neno lililoandikwa, (bali si hilo Neno lililofunuliwa). Huu ulikuwa ni wakati wa yale matengenezo. Lakini msiogope enyi kundi dogo, Mungu alisema, "Nitarudisha," na matengenezo haya yalikuwa yakienda kuwa ndiyo mwanzo wake. Yeye alikuwa yuaenda (kulingana na ahadi Yake) kulirudisha kanisa kutoka kwenye fumbo la Shetani katika zile Zama za Giza aliingize katika Fumbo la Mungu ambalo walikuwa nalo wakati wa Pentekoste na katika ile miaka michache ya kwanza ya kuweko kwa kanisa.

Sasa iweni waangalifu, na mlipate jambo hili. Inasemwa katika aya hii ya pili niliyosoma, "Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu." Unajua hasa maana ya „hayajatimilika" ni nini? Ni „kutomalizika." Wakati huu ulikuwa ni wakati usiotimilika. Ulikuwa ni mwanzo tu wa kurudi. Hiyo ndiyo sababu nilisema Biblia iliuita Matengenezo_si kurudishwa. Ulikuwa umeshaanza kwa fundisho la kuhesabiwa haki ambalo lilimaanisha wokovu wote ulikuwa ni kazi ya Mungu. Loo! jinsi Luther alivyohubiri mamlaka ya Mungu na kuteuliwa. Yeye alijua yote yalikuwa ni kwa neema. Alilitenganisha kanisa na utawala wa serikali ya kanisa. Alizivunja sanamu. Alitupilia mbali kwenda kutubu kwa makasisi. Alimshambulia papa hadharani. Hali ilikuwa nzuri sana, alivyoanza, bali Mungu alikuwa ameshasema miaka 1500 kabla, "Luther, utaanzisha mambo, lakini wakati wako hutayaona yametimilika yote, ninaachia jambo hilo kwa siku za baadaye." Haleluya, Mungu wetu anatawala! Yeye anajua mwisho kutoka mwanzo. Naam, Luther alikuwa ni mjumbe Wake. Haikuonekana kama ndivyo ilivyo, tunapoyachunguza makosa yake. Lakini kulikuweko na mtu aliyeitwa Yona, yeye naye alikuwa na makosa katika maisha yake. Yeye alikuwa ni nabii ingawa mimi na wewe huenda tusitake kusema hivyo juu ya msingi wa vile alivyotenda. Lakini Mungu anawajua hao walio Wake na anafanya apendavyo na kama tu alivyofanya na Yona. Yeye alifanya alivyopenda na Luther katika wakati ule, Naye atafanya apendavyo hata ukamilifu wa dahari.

Sasa huu ulikuwa ni wakati usiotimilika. Ulikuwa ni wakati wa matengenezo. Lakini hivyo ndivyo Mungu alivyotaka uwe. Ninataka kuwaelezeeni jambo hilo jinsi vile nilivyofanya kwa ndugu mzuri sana wa Kiluteri ambaye ni mkuu wa seminari nzuri sana huko pande za Magharibi. Nilikuwa nimekaribishwa nyumbani kwake kula naye chakula cha jioni na nimzungumzie kuhusu Roho Mtakatifu. Alikuwa ametatanishwa na mambo mengi naye akaniambia, "Sisi Waluteri tuna kitu gani?"

Nikasema, "Vema, mna Kristo."

Akasema, "Tunataka Roho Mtakatifu. Unafikiri tunaye?"

Nikasema, "Kwa uwezekano, mnaamini mpate kumpokea Yeye."

Akasema, „Una maana gani, kwa uwezekano? Tuna njaa ya Mungu. Tulisoma kitabu fulani juu ya Pentekoste na karama za Roho, kwa hiyo baadhi yetu tukaruka kwa ndege mpaka California kuonana na mwandishi wake. Tulipofika huko alitwambia ya kwamba ingawa yeye alikuwa amekiandika kitabu hicho, yeye hakuwa na hizo karama. Sasa wakati tulipoona karama zikitenda kazi katika huduma yako tulitaka kuzungumza na wewe, kwa maana hapana budi una fununu nazo."

Sasa seminari ya ndugu huyu iko huko bara na imezungukwa na ekari nyingi za mashamba ambamo wanafunzi wanaweza kufanya kazi na hivyo basi kujilipia masomo yao ya chuo. Pia ana viwanda vinavyoendana na shamba hilo kwa ajili ya kutoa kazi zaidi. Kwa hiyo nikitumia mashamba yake ili kueleza hoja yangu nilisema, "Siku moja alitokea mtu aliyetoka akaenda shambani mwake akapanda shamba la mahindi. Aling"oa visiki, akaondoa miamba, akalima na kutifua udongo halafu akapanda mahindi yake. Kila asubuhi aliangalia shambani; lakini asubuhi moja badala ya shamba tupu aliona utitiri wa vijani vinavyoota. Akasema, "Mungu na asifiwe kwa ajili ya shamba langu la mahindi." Ndipo nikamwuliza, "Je!

mtu huyo alikuwa na mahindi?"

Akasema, "Vema, kwa namna fulani alikuwa nayo."

Nikasema, "Kwa uwezekano, ndiyo; na hiyo ilikuwa ni ninyi Waluteri katika yale matengenezo, mkichomoza majani yenu, mnaona? Mahindi yakaanza kukua. (Baada ya kuoza ardhini katika zile Nyakati za Giza). Baada ya pingili kadha kukawa na mabua mazuri na makubwa, na siku moja kishada cha hariri kikatokea. Hicho kishada cha hariri kiliinama kikayatazama majani yaliyokuwa chini na kusema, "Enyi Waluteri wa kale baridi hamna lo lote. Tuangalieni sisi, sisi ndio wenye kuzaa, wamishenari mashuhuri. Siku yetu ni kipindi cha umishenari." Wakati huo wa kishada ulikuwa ni Wakati wa Wesley. Walikuwa wamishenari mashuhuri sana na hata walitushinda sisi katika wakati wetu. Huo wakati ulifanya nini? Ulitawanyika kama chavua katika upepo.

"Sasa hatua inayofuata ni nini? Kwa mpangilio wa mawazo, tunafikiri huko ndiko kutengenezwa kwenyewe hasa kwa nafaka na kuvuna—mzunguko kamili. Lakini sivyo ilivyo. Kuna hatua nyingine. Hatua hiyo ni wakati ganda au makapi yanapotengenezwa kufunika mbegu. Na hilo ndilo hasa lililotukia katika mzunguko huu wa Kiroho. Mwanzoni mwa karne ya ishirini, katika mwanzo wa Wakati wa Laodikia, kulikuwa na imani iliyoenea sana ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa anashuka vile vile tu kama alivyofanya wakati wa Pentekoste. Watu walikuwa wakinena kwa lugha na kudai kubatizwa na Roho Mtakatifu wakiwa na ushuhuda wa kunena kwa lugha. Lakini nimetembea kwenye mashamba ya nafaka mara nyingi, na humo mwishoni mwa kiangazi nimekonyoa vichwa vya ngano na kuvisugua katika mkono wangu nipate punje, lini nilishangaa HAPAKUWEPO NA PUNJE YO YOTE YA NGANO KATIKA KAPI HILO, INGAWA KWELI ILIONEKANA KANA KWAMBA NGANO ILIKUWEPO. Hii ni picha kamilifu ya unaoitwa ufufuo wa Wapentekoste.

Na kwamba huu ni ukweli uliothibitishwa inaonekana kwa kuwa watu hawa WALIUNDA MADHEHEBU JUU YA FUNDISHO FULANI na wakajifunga moja kwa moja kama yalivyofanya madhehebu yaliyowatangulia, ikithibitisha ya kwamba badala ya kuwa mbegu halisi, walikuwa ni makapi ama kifuniko cha kuikinga punje ya ngano ambayo inapaswa kuja. Wakati huu wa makapi ulikuwa ni kipindi cha hatari ambacho Yesu alinena habari zake katika Mat. 24:24, "kuwapoteza walio wateule kama yamkini." Loo! mwanadamu alijisikia ya kwamba ganda hili, huo eti uitwao Wakati wa Kipentekoste ulikuwa ndio mbegu halisi. Lakini ulithibitisha kuwa ni mbebaji tu wa kubeba uhai kuupeleka katika wakati ambapo kurudishwa kwa kweli kunakuja na Bibi-arusi Ngano anadhihirishwa katika nguvu zilizonenwa na Ezekieli 47:2-5,

> *"Ndipo akanileta nje kwa njia ya lango upande wa kaskazini, akanizungusha kwa njia ya nje mpaka lango la nje, kwa njia yake iliyoelekea mashariki; na tazama, maji yalitoka upande wa kuume.*
>
> *Na alipotoka mtu yule, mwenye uzi wa kupimia mkononi mwake, kwenda masharikini, akapima dhiraa elfu, akanivusha maji yale; maji yakafika mpaka viweko vya miguu.*
>
> *Kisha akapima dhiraa elfu, akanivusha maji yale, maji yakafika mpaka magoti. Kisha akapima dhiraa elfu, akanivusha, maji yakafika mpaka viuno.*
>
> *Kisha akapima dhiraa elfu, yakawa mto nisioweza kuuvuka; maana maji yamezidi, maji ya kuogelea, mto usiovukika."*

*"Na jinsi jambo hilo lilivyofanyika ilikuwa ni kwa mapenzi makamilifu ya Mungu na mipango Yake.* Waluteri walikuwa na Roho Mtakatifu kwa uwezekano chini ya kuhesabiwa haki; Wamethodisti walikuwa Naye kwa uwezekano chini ya utakaso na leo amerudishwa, kurudishwa_Roho Mtakatifu yuko hapa."

*"Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa."*

Sasa mawazo yaliyoelezewa katika maneno hayo mawili, "akeshaye" na "ukayaimarishe" ni haya. Kukesha hakuna tu wazo la kuwa macho bali kuwa mwangalifu. Kuwa vinginevyo kunadokeza hatari na hasara. Kuimarisha kunamaanisha zaidi ya kutia nguvu tu, linamaanisha kutengeneza na kusimamisha kwa ajili ya kudumu kwa muda mrefu. Amri hizi mbili zinahusu UKWELI uliosalia ambao wenyewe uko tayari ama "karibu" kufa. Tamshi hili la Roho linakuja mbele zangu kama mfano. Kundi la watumwa, waliofungwa kabisa kimwili na kimaadili wameasi na kutoroka kutoka kwa waliowashika (kwa kweli hivyo ndivyo Sardi inavyomaanisha: waliotoroka). Wanafuatiwa na ushindi wao mkubwa na mzuri sana karibu wote umepotea. Hawajashikwa tena bado, lakini karibu yote yanayoweza kusemwa ni kwamba wametoroka_si kutoroka kabisa kama wengine wao walivyokuwa kulingana na Neno. Walikuwa wamepoteza sehemu kubwa ya uhuru wao.

Sasa Bwana anasema, "Kwa uwezekano mmerudi utumwani; angalieni msirudi. Ili kujihami msirudi iweni macho na dumuni mkikesha daima kuhusu mambo ya utumwa wenu la sivyo mtapoteza yote. Jiimarisheni sasa katika yale yaliyosalia hivi kwamba mtaweza kuimarisha kabisa yale mliyo nayo na kwa hiyo mhakikishe hamtapoteza kitu katika siku zijazo. Hii itakuwa ni nafasi yenu kutimiza yale ambayo hamjatimiza." Lakini je! wao waliendelea? La bwana. Hawakuisikiliza sauti ya Roho na wakati mwingine wa

kanisa ukaingia utumwani na kwa hiyo Mungu akawainua wengine ambao wangefanya mapenzi Yake. Mungu aliyapita madhehebu ya Kiluteri kama alivyofanya na mengine yote, nayo hayatarudi tena. Ilibidi Mungu kuendelea na katika wakati mwingine mpya aongezee kweli zaidi na kurudishwa kwingine zaidi.

**HUKUMU**

Ufunuo 3:3,

> *"Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako."*

Ninataka kusoma tafsiri nyingine (Wuest) ya aya hii,

> *"Endelea kukumbuka, basi, umepokea kwa njia gani (ukweli kama akiba ya kudumu) na jinsi ulivyolisikia (hilo) na kulilinda (hilo), na ubadilishe nia mara moja."*

Ni dhahiri sana kutoka katika aya hii ya kwamba Mungu alikuwa amewapa kweli kama akiba ya kudumu. Ilipokewa na ni yao na hawawezi kunyang"anywa. Kinachobaki sasa ni kuona kile watakachofanya nayo, kama wataiheshimu ama hawataiheshimu. Na hiyo ni kweli. Wamekwishapewa msingi wa kweli wa Injili yote, "Mwenye haki ataishi kwa imani", *"Wokovu ni wa Bwana."* Walikwishasikia kweli ya Biblia ambayo iliyatupilia mbali mafundisho ya Rumi na kuyapuuza kabisa mamlaka yote ya papa. Walijua kweli kwamba kanisa haliokoi. Walifahamu meza ya Bwana. Walikuwa na nuru juu ya ubatizo wa maji. Waliondoa sanamu. Kweli? Mbona hakujawahi kuwepo na wakati wenye watu wengi zaidi waliokuwa na nuru nyingi namna hiyo ya kuangaza. Walikuwa na mwangaza wa kutosha kuharibu kabisa ule utaratibu wa kale au kuanza upya na kumwacha Mungu awaongoze, mstari juu ya mstari, na kanuni juu ya kanuni. Walipokea ile kweli. Waliitaka na waliisikia.

Lakini swali lilikuwa, walisikiaje? Waliisikia ili kusudi wajenge juu yake ama ilikuwa ni msimamo ule ule ambao Wayunani wengi walikuwa nao_jambo fulani la kuhojiana na kutoa nadharia juu yake? Kwa kweli Neno zuri la kweli lilikuwa linasikiwa kwa njia ya kielimu, badala ya matendo yanayofaa, kwa kuwa Mungu alikuwa akidai wabadilishe nia zao kulihusu. Kama hili ni Neno la Mungu ambalo kweli ndilo, basi halina budi kutiiwa. Kutolitii kungeleta hukumu. Wakati walinzi wa hekalu takatifu walikutwa wamelala usingizi, walichapwa kisha mavazi yao yakachomwa moto. Bwana atawafanya nini hao ambao katika wakati huu wamelegeza ulinzi wao?

*"Nitakuja kwako kama mwivi."*

Sardi ya kale daima ilisumbuliwa na maharamia walioshuka wakawavamia toka vilimani na kuwateka watu nyara. Hivyo basi wao walijua vizuri sana tu yale Roho aliyokuwa anasema ya kwamba kule kuja kwa Bwana ni kama mwizi. Kuwa macho na matayarisho ndiko pekee kutakakotosheleza kuwa tayari kwa ajili ya kuja Kwake. Sasa tunajua ya kwamba huu ni ujumbe kwa ajili ya ule mzabibu wa uongo, kwa maana kuja kwa Bwana kutakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Wale wanane waliookolewa walikuwa wanajua vyema habari za gharika ijayo, na kwa kuwa walijua wao walijiweka tayari na wakaokolewa. Lakini ulimwengu wa wasiomcha Mungu ulifutiliwa mbali. Ingawa kila siku walikutana na watu wenye haki na walisikia ile kweli, waliikataa mpaka wakachelewa. Wale watu wa kimwili kabisa katika wakati ule wa kale ni mfano wa Wakristo wa kawaida wa siku hizi ambao maisha yao yamejaa mambo ya dunia, na wanayafurahia hivi kwamba hawana shauku na mambo ya Kiroho, na wala hawana habari kabisa nayo, wala hawajawa tayari kwa ajili ya kuonekana Kwake.

**SIFA**

Ufunuo 3:4,

> *"Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu; nao watakwenda pamoja Nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili."*

Bila shaka neno „majina" linamaanisha „watu" kama isemavyo katika Matendo 1:15 kuhusu wale waliokuwa katika chumba cha juu, "jumla ya majina ilipata 120." Lakini kwangu mimi lina maana zaidi kuliko tu ya kuwawakilisha watu; linadhihirisha ile kweli ambayo imewekwa katika kila wakati ambayo ilinenwa kwetu kwa mkazo mkuu na Bwana wetu. Ni hili: muundo wa kanisa wa nyakati hizi umeundwa kwa mizabibu miwili, wa kweli na wa uongo. Mungu katika kusudi la mamlaka Yake makuu ameyaweka yote pamoja, akiyaita kanisa.

Angalia katika wakati huu jinsi Yeye alivyowakemea akisema, *"kwa kanisa lililoko"*—si "makanisa yaliyoko" Sardi—lakini akiyalundika pamoja—"kanisa lililoko"... *"Najua matendo yako … umekufa … kazi zako hazijatimilika …"* Halafu anaendelea—"Una (kanisa hili lililoko Sardi) watu wachache wazuri, na si wabaya kama walivyo wengi. Hawa wanatembea katika mavazi safi na wao wananistahili Mimi." Sasa watu hawa waliokuwa watakatifu wa kweli wa Mungu walikuwa wanatembea "wote wakimpendeza Bwana." Mavazi yao yalikuwa safi. Mnaona katika siku zile hayo mavazi yaligusa ardhi na kuzoa vumbi na

uchafu. Hawa waliangalia jinsi walivyoenenda hivi kwamba wasipotoshwe na ulimwengu. Walikuwa katika Roho na wakitembea katika Roho. Walikuwa watakatifu na wasio na lawama mbele Zake. Hivyo walikuwa wanatimiza kusudi lao kwa kuwa hivyo ndivyo Efe. 1:4 inavyosema ndilo kusudi la Mungu kwa ajili yetu, "ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele Zake."

Sasa kutokana na aya hii inayoonyesha wateule wa Mungu kwamba ni "Majina Machache," unaweza kuona dhahiri yale tuliyokuwa tukifundisha kuhusu wakati huu. Ulikuwa umechafuka sana. Ulikuwa HAUJATIMILIKA. Ulikuwa umegawanyika katika njia nyingi, na Mungu akaukemea karibu wote. Ulikuwa dhaifu na mgonjwa na karibu kufa. Haukuwa wakati wa fahari kama vile wanahistoria Waprotestanti wenye nia za kimwili walivyojaribu kuufanya. Mtazamo mmoja wa haraka wa mti huo uliona kuwa umeoza na umeshikwa na ugonjwa, hauna majani wala matunda isipokuwa kwa matunda machache yaliyoumbuka na yaliyoliwa na wadudu ambayo yalikuwa yakianguka haraka ardhini. Lakini ngoja kidogo! Angalia kwa makini. Kule juu, kwenye nuru ya jua, kulikuwa na „malimbuko"—"Majina Machache"—waliokuwa wakamilifu katika Yeye kwa maana walizaliwa Naye, wamejazwa Naye na wakitembea Naye kwa Neno Lake.

Asante Mungu kwa ajili ya 'hao wachache.'

*"Nao watakwenda pamoja Nami."*

Hicho ndicho ambacho Mungu anasema atawapa kwa ajili ya mwenendo huu mnyofu. Hiyo ni sehemu ya urithi wao ambao Yeye amewawekea. Kama walikuwa tayari kutembea pamoja Naye kupitia kwenye taabu na mitego ya maisha na kuwa waaminifu Kwake, Yeye alikuwa anaenda kuwapa thawabu. Yeye hasahau taabu yetu ya upendo. Mungu daima atatujazi kwa ajili ya jitihada zetu za kumfurahisha Yeye.

Naam, walikuwa wametembea ulimwenguni wala hawakuwa wameshiriki mambo yake. Hawakuwa wameziachilia taratibu za ulimwengu ziwashinde. Wakati hayo majina maarufu sana ya wakati huo yalipokuwa yamejisalimisha kwenye upendeleo wa serikali na wakachagua mambo ya kisiasa badala ya mambo ya Kiroho nao walikuwa wanaenda zao kurudi ulimwenguni, hawa wachache walilitetea Neno la Mungu, na hivyo basi wakamheshimu Bwana. Sasa Yeye naye angewaheshimu vivyo hivyo. Kwa kuwa watakwenda pamoja Naye hali wamevaa mavazi meupe. Walikuwa wamejitambulisha Naye duniani na sasa Yeye atajitambulisha pamoja nao katika Yerusalemu Mpya. Na ni jinsi gani kujitambulisha huko kutakavyokuwa kuzuri! Linanifanya nishangilie na hata hivyo linanifanya nilie kufikiria juu ya kujidhili Kwake, kwa kuwa utaona kwamba Yeye havai rangi nyingine tofauti na watakatifu, kama ambavyo viongozi wa dunia wangefanya. La, wao ni kama Yeye; Yeye ni kama wao. Wao ni kama Yeye, kama vile Yohana alivyosema; kwa kuwa "wanamwona Yeye kama alivyo."

*"Kwa kuwa wamestahili."* Unatambua ni Nani anayesema jambo hili? Ni Yesu, Yeye Anayestahili, Mwenyewe. Huyu Ndiye pekee Ambaye amehesabiwa kuwa anastahili kukitwaa kile kitabu kutoka katika mkono Wake Yeye aliyeketi kwenye kiti cha enzi. Na sasa Huyu Anayestahili anawaambia watakatifu Wake, "Ninyi mmestahili." Huyu hapa Mmoja, Yule pekee anayestahili kuwa hakimu, (na kwa kweli hukumu yote amekabidhiwa Yeye,) Naye anasema, "Nyinyi mmestahili."

Maneno haya yanashangaza sana kama yale maneno ya Rum. 8:33b,

"Mungu anasema mimi ni mwenye haki."

(Tafsiri ya Way.) Pale katika nuru nyeupe ya haki ya Mungu, isikie sauti tamu ya Yesu anaposema, "Hawa ni Wangu. Wao ni wenye haki. Wanastahili. Watatembea pamoja Nami katika mavazi meupe."

**AHADI KWA MSHINDI**

Ufunuo 3:5,

> *"Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika Kitabu cha Uzima, lakini nitalikiri jina lake mbele za Baba Yangu, na mbele ya malaika Zake."*

> *"Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe."*

Hili kwa kweli ni marudio ya aya ya 4, ambapo pametajwa hao wachache ambao hawajayatia mavazi yao uchafu. Tulikuwa na msemo miaka mingi iliyopita ambao bila shaka ulitolewa kutoka kwenye aya hii. Ulikuwa, "Msichafue sketi zenu." Msemo huo ulimaanisha: usihusike na mambo yasiyo wazi; wengine watahusika na wewe huenda ukashawishika kuhusika, ama mtu fulani hata anaweza kujaribu kukuhusisha; lakini kaa mbali na jambo lote kwa kuongoza katika njia iendayo mbali na jambo hilo. Sasa Mungu atawapa thawabu wale wanaofuata ushauri huu. Watavalishwa mavazi meupe kama vile Yeye alivyovaa mavazi meupe. Petro, Yakobo na Yohana walimwona kwenye Mlima wa Kugeuka Sura na mavazi Yake yalikuwa meupe kama nuru. Hivyo ndivyo watakatifu watakavyovalishwa. Mavazi yao yatakuwa yaking"aa, meupe sana.

Mnajua tunaishi katika wakati wa mwisho. Wakati huu ndio ambapo makanisa yataungana. Na kama

vile ambavyo hata sasa yanatawala siasa za ulimwengu, hivi karibuni yatatawala uchumi wa dunia. Basi, kama wewe si mfuasi wa shirika la makanisa ulimwenguni, hutaweza kuuza wala kununua. Utapoteza yote. Wale wanaodumu kuwa waaminifu kwa Mungu na kuyaweka mavazi yao meupe yasichafuliwe na huu „utaratibu wa ulimwengu" wa mashirika ya kanisa wataachwa bila mali. Wataletewa jaribu kubwa sana wapate kujisalimisha. Wahubiri watajisalimisha kwa kisingizio cha kwamba watamtumikia Mungu wakiwa ndani ya utaratibu wa mnyama mpinga-kristo. Watajisalimisha kwa sifa za ule ulaghai na ushawishi wa serikali ya kanisa. Nao watu watawafuata hawa wachungaji wa uongo moja kwa moja hata machinjioni. Lakini hukumuni wote watakutwa uchi. Hawatapewa hayo mavazi meupe; wala hawatatembea pamoja Naye. Huwezi kutembea umevaa mavazi ya ulimwengu ambayo yana mawaa, huku ukiwa umeshikana mikono na ibilisi, na halafu utazamie kuwa pamoja na Mungu. Ni wakati wa kuamka na kuisikia sauti ya Mungu ikisema kwa sauti kuu, "Tokeni kwake (dini ya kimadhehebu) enyi watu Wangu, msije mkashiriki dhambi zake, msije mkapokea mapigo yake." Amina. Mungu ananena. Jiepusheni na dini za ulimwengu huu kama vile mnavyojiepusha na tauni. Acheni kutembea pamoja na ulimwengu na myafanye mavazi yenu meupe kwa toba na damu ya Mwana-Kondoo. Lakini fanyeni jambo hilo sasa, kwa maana kesho inaweza kuwa umechelewa.

*"Na yeye ashindaye, sitalifuta jina lake katika Kitabu cha Uzima."*

Mara nyingine tena tunafikia sehemu ngumu sana ya Neno. Aya hii ikiangaliwa kwa juu-juu itatumiwa na Waarminia na Wakalvini pia ifae mashauri yao.

Waarminia watasema kwa uthabiti ya kwamba aya hii bila shaka inafutilia mbali Yon. 6: 37-44,

> *"Wote anipao Baba watakuja Kwangu; wala ye yote ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe.*
>
> *Kwa kuwa Mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi Yangu, bali mapenzi Yake Yeye aliyenipeleka.*
>
> *Na mapenzi ya Baba Yangu aliyenipeleka ni haya, ya kwamba katika wote alionipa nisimpoteze hata mmoja, bali nimfufue tena siku ya mwisho.*
>
> *Basi Wayahudi wakamnung"unikia, kwa sababu alisema, Mimi ni chakula kilichoshuka kutoka mbinguni.*
>
> *Wakasema, Huyu siye Yesu, Mwana wa Yusufu, ambaye twamjua babaye na mamaye? Sasa asemaje huyu, Nimeshuka kutoka mbinguni?*
>
> *Basi Yesu akajibu, akawaambia, Msinung"unike ninyi kwa ninyi.*
>
> *Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; Nami nitamfufua siku ya mwisho."*

Uarminia unafanya mapenzi ya Baba, si kusudi la mamlaka kuu, lakini ni shauku tu ya ridhaa huyo Baba anaposimama huko nyuma aone yale watu wote wanayofanya na karama Zake za kweli na za neema, na hata uzima wa milele.

Wakalvini hawaoni jambo hilo. Wanaona katika aya hii faraja kubwa sana iliyotolewa kwa watakatifu wanaoteseka, waliolemewa na mizigo, ya kwamba haidhuru nyakati hizo ni za uovu namna gani, jinsi mateso yalivyo ya kutisha, kwa sababu mshindi ni mmoja, "anayeamini ya kwamba Yesu ni Kristo," jina lake halitaondolewa kwenye kile kitabu. Wengine wanasema pia ya kwamba „Kitabu hiki cha Uzima" si „Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo." Lakini kama kawaida, wakati mtu anapoangalia aya kwa juujuu, yeye anaondoka akiwa na ufahamu wa kijuujuu.

Uwezekano wa kuondolewa kwa jina kutoka kwenye rekodi za Mungu kunahitaji zaidi ya somo la juujuu, kwa sababu hadi kufikia wakati huu karibu wanafunzi wote wamefikia kwenye uamuzi ya kwamba Mungu huweka majina ya wale waliozaliwa mara ya pili katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo wakati wa kuzaliwa kwao upya; na kama kwa sababu yo yote jina hilo litapaswa kuondolewa, sehemu hiyo kwenye rekodi itakuwa ni tupu tu kama ilivyokuwa kabla ya jina halijaandikwa pale. Hili ni asilimia mia moja kinyume na yale hasa Neno linayofundisha.

Katika mwanzo kabisa wa somo letu, hebu na ijulikane ya kwamba hakuna Andiko HATA MOJA linalofundisha ya kwamba Mungu hivi sasa anaandika orodha ya majina. Jambo hili lilifanywa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kama tutakavyoonyesha hivi punde. Pia, si swali la sisi kujihusisha na makundi mawili ya watu ambao wote walikuwa na nafasi ya kupokea uzima wa milele, ambapo kundi moja liliupokea na majina yao yakaandikwa kwenye orodha ambapo wale wengine waliokataa hawakuandikwa majina yao. Kwa kweli tutaonyesha kwa Maandiko ya kwamba umati mkubwa wa watu ambao hata hawakuzaliwa mara ya pili wataingia katika uzima wa milele. Ingawa hili linaweza kusikika ni jambo geni, hakika ni la kweli. Pia tutaonyesha ya kwamba kuna kundi la watu ambao majina yao, baada ya kuandikwa kwenye orodha hiyo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, MAJINA HAYO HAYAWEZI

KUONDOLEWA KWA HALI YO YOTE; lakini pia tutaonyesha ya kwamba kundi lingine AMBALO MAJINA YAO YALIKUWA KWENYE ORODHA HIYO KABLA YA KUWEKWA MISINGI YA ULIMWENGU MAJINA YAO YATAFUTILIWA MBALI.

Kwanza, hakuna msingi kwa madai kwamba „Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo" si sawa na „Kitabu cha Uzima." Kitabu cha Uzima kinaweza kuitwa Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ama Kitabu cha Uzima cha Kristo, ama hata Kitabu Chako na Kitabu cha Walio Hai. Ni majina tu yaliyoandikwa ndani yake.

Ufunuo 13:8,

> *"Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, (huyo mnyama) kila ambaye jina lake halikuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia."*

Ufunuo 17:8,

> *"Yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi wasioandikwa majina yao katika Kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako."*

Ufunuo 20:12-15,

> *"Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele za Mungu; na vitabu vikafunguliwa; na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha Uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yote yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.*
>
> *Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.*
>
> *Mauti na kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili.*
>
> *Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika Kitabu cha Uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."*

Mnaweza kuona ya kwamba ingawa kuna vitabu vingine vilivyotajwa, daima kuna kutajwa kwa kitabu KIMOJA kilicho na majina. Katika Ufunuo kinaitwa „Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo", ama „Kitabu cha Uzima."

Sasa kitabu hiki kiko wapi? Luka 10:17-24,

> *"Ndipo wale sabini waliporudi tena kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa Jina Lako.*
>
> *Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme.*
>
> *Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru,*
>
> *Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.*
>
> *Saa ile ile Yesu alishangilia kwa Roho, akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili; umewafunulia watoto wachanga; Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyokupendeza.*
>
> *Nimekabidhiwa vyote na Baba Yangu, wala hakuna amjuaye Mwana ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia.*
>
> *Akawageukia wanafunzi Wake, akasema nao kwa faragha, Heri macho yaonayo mnayoyaona ninyi:*
>
> *Kwa kuwa nawaambia ya kwamba manabii wengi na wafalme walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi wasiyasikie."*

Kitabu cha Uzima bila shaka kiko mbinguni, na kitatokea kwenye ile hukumu kuu ya Kiti Cheupe cha Enzi. Katika aya hizi Yesu alisema ya kwamba MAJINA yao yaliandikwa mbinguni. Yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima, kwa maana humo ndimo majina yanamowekwa. Yesu alikuwa akizungumza na wale sabini (aya ya 17), lakini alikuwa pia akizungumza na wale kumi na wawili (aya ya 23). Hawa wote walikuwa wakifurahi ya kwamba pepo walikuwa wakiwatii katika Jina la Yesu. Jibu la Yesu lilikuwa,

"Msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii, bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni (Kitabu cha Uzima)." Utaona hapa ya kwamba Yuda alikuwa ni mmoja wa wale waliokuwa wanatoa pepo katika Jina la Yesu, lakini tunajua ya kwamba yeye alikuwa ni shetani, mwana wa upotevu.

Yohana 6:70-71,

> *"Yesu akawajibu, Je! Mimi sikuwachagua ninyi thenashara, na mmoja wenu ni shetani? Alimnena Yuda Iskariote, mwana wa Simoni: maana huyo ndiye atakayemsaliti, naye ni mmojawapo wa wale thenashara."*

Yohana 17:12,

> *"Nilipokuwapo pamoja nao duniani, Mimi naliwalinda kwa Jina Lako: wale ulionipa, nikawatunza, wala hapana mmojawapo wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu: ili Andiko litimie."*

Yohana 13:10-11, 18,

> *"Yesu akamwambia, Yeye aliyekwisha kuoga hana haja ila ya kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote, nanyi mmekuwa safi, lakini si nyote.*
>
> *Kwa maana alimjua yeye atakayemsaliti; ndiyo maana alisema, Si nyote mlio safi.*
>
> *Sisemi habari za ninyi nyote: nawajua wale niliowachagua: lakini Andiko lipate kutimizwa, yeye alaye chakula pamoja Nami ameniinulia kisigino chake."*

Sasa kama lugha ina maana yo yote hata kidogo hatuna budi kukubali ya kwamba Yuda alichaguliwa na Yesu (Yn. 13:18), lakini yeye hakuwa safi. (Yn. 13:10-11), pia pia Yesu alipewa Yuda na Baba Yake. Yohana 17:12. *(Hebu na ijulikane hapa kwamba kule "kuchaguliwa" na kutoa ni jambo lile lile liendalo sambamba sambamba kabisa na kama vile katika mfano wa Musa na Farao, Yakobo na Esau, kwa maana ingawa Esau na Farao walijulikana wote wawili tangu zamani, walikusudiwa ghadhabu, ambapo mwisho wa Musa na Yakobo ulikuwa ni kutukuzwa.* I Petro 2:8-9a inaonyesha wote waliokataliwa na walioteuliwa "kwa maana hujikwaza kwa Neno lile, wasiliamini: nao waliwekwa kusudi wapate hayo. Bali ninyi ni mzao mteule.") Yuda alihesabiwa pamoja na wale kumi na wawili na kwa kweli alikuwa na sehemu pamoja nao katika huduma iliyotangulia Pentekoste.

Matendo 1:16-17,

> *"Ndugu, ilipasa Andiko litimizwe, alilolinena Roho Mtakatifu zamani kwa kinywa cha Daudi, katika habari za Yuda, aliyewaongoza wao waliomkamata Yesu.*
>
> *Kwa sababu alikuwa amehesabiwa pamoja na sisi, akapata sehemu ya huduma hii."*

Sehemu ambayo Yuda aliipata kati ya wale thenashara halafu akaipoteza haikuwa ndogo kuliko huduma za hao wengine kumi na mmoja, wala haikuwa huduma ngeni ya kiibilisi iliyoingizwa kati ya huduma za hao wengine.

Matendo 1:25,

> *"Ashike mahali katika huduma hii na utume huu, alioukuosa Yuda, aende mahali pake mwenyewe."*

*Yuda, ambaye alikuwa shetani, alipoteza huduma ya Roho Mtakatifu aliyopewa na Mungu, ndipo akajiua na AKAENDA MAHALI PAKE MWENYEWE.* Jina lake hata lilikuwa katika Kitabu cha Uzima. Lakini jina lake lilifutiliwa mbali.

Sasa kabla hatujalifuatilia wazo hili juu ya Yuda, hebu na turudi nyuma katika Agano la Kale tuone mahali ambapo Mungu alitenda jambo lile lile. Katika Mwa. 35:23-26, wana wa Yakobo walikuwa thenashara na majina yao yalikuwa kama ifuatavyo: Reubeni, Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, na Zabuloni; Yusufu na Benyamini; Dani na Naftali; Gadi na Asheri. Ukoo wa wana hawa thenashara ukawa yale makabila kumi na mawili ya Israeli isipokuwa Yusufu hakuwa na kabila lililoitwa kwa jina lake, kwa maana katika mawazo ya mbele ya Mungu ilikuwa kuwe na makabila kumi na matatu, na wale wana wawili wa Yusufu walipewa heshima ya kuyafanya yale kumi na mawili kuwa kumi na matatu. Mnajua, bila shaka, ya kwamba jambo hili lilikuwa la lazima kwa kuwa Lawi alitengwa kwa Mungu kwa ajili ya ukuhani. Kwa hiyo wakati Israeli walipoondoka Misri na Mungu akawapa ile hema jangwani, tunaona kabila la Lawi likiwahudumia makabila kumi na mawili ambayo majina yao ni Reubeni, Simeoni, Isakari, Yuda, Zabuloni, Benyamini, Dani, Naftali, Gadi, Asheri, Efraimu na Manase. Hiyo ndiyo taratibu ya majina ya jeshi lao katika Hes. 10:11-28. Hakuna kutajwa kwa Yusufu au Lawi. Lakini tunapoangalia Ufu. 7:4-8, ambapo inasema "walitiwa muhuri watu mia na arobaini na nne elfu katika KILA kabila la wana wa Israeli," linawaorodhesha namna hii: Yuda, Reubeni, Gadi, Asheri, Naftali, Manase, Simeoni, Lawi, Isakari,

Zabuloni, Yusufu, Benyamini. Tumerudi kwenye makabila kumi na mawili huku Lawi na Yusufu wametajwa miongoni mwao, lakini Dani na Efraimu wanakosekana.

Swali sasa linazuka, ni kwa sababu gani haya makabila mawili yalifutiliwa mbali? Jawabu liko katika Kum. 29:16-20,

> *"Kwani mwajua tulivyoketi nchi ya Misri, na tulivyokuja katikati ya mataifa hayo mliyopita katikati yao;*
>
> *Nanyi mliona machukizo yao, na sanamu zao, miti na mawe, fedha na dhahabu, zilizokuwako kwao:*
>
> *Asiwe mtu katikati yenu, mume wala mke, wala jamaa, wala kabila, ageukaye moyo wake leo amwache Bwana, Mungu wetu, kwenda kuitumikia miungu ya mataifa hayo; lisiwe katikati yenu shina lizaalo uchungu na pakanga;*
>
> *Ikawa asikiapo maneno ya laana hii, ajibarikie mtu huyo moyoni mwake, na kusema, Nitakuwa katika amani, nijapotembea katika upotoe wa moyo wangu, kwa kuangamiza mbichi na kavu;*
>
> *Bwana hatamsamehe mtu huyo, lakini wakati huo hasira ya Bwana na wivu Wake vitafuka moshi juu ya mtu yule, na laana yote iliyoandikwa katika kitabu hiki itamkalia juu yake, na Bwana atalifuta jina lake chini ya mbingu."*

Hapa imetangazwa laana dhidi ya ibada za sanamu, ama uasherati wa kiroho. Kabila ambalo liligeukia ibada za sanamu ilibifi jina lake lifutwe. Na historia ya hayo makabila mawili ambayo majina yao yalifutwa kwa sababu ya ibada za sanamu inapatikana katika I Waf. 12:25-30,

> *"Ndipo Yeroboamu akajenga Shekemu katika milima ya Efraimu, akakaa huko; akatoka huko akajenga Penueli.*
>
> *Yeroboamu akasema moyoni mwake, Basi ufalme utairudia nyumba ya Daudi:*
>
> *Kama watu hawa wakipanda kwenda kutoa dhabihu katika nyumba ya Bwana huko Yerusalemu, ndipo mioyo ya watu hawa itamrudia bwana wao, yaani Rehoboamu, mfalme wa Yuda, nao wataniua mimi, na kumrudia Rehoboamu, mfalme wa Yuda.*
>
> *Kwa hiyo mfalme akafanya shauri, akafanyiza ng"ombe wawili wa dhahabu, akawaambia watu, Ni vigumu kwenu kupanda kwenda Yerusalemu; tazama, hii ndiyo miungu yenu, Enyi Israeli, iliyowapandisha kutoka nchi ya Misri.*
>
> *Akamweka mmoja katika Betheli, na wa pili akamweka katika Dani. Jambo hili likawa dhambi: maana watu walikwenda kuabudu mbele ya kila mmoja, hata huko Dani."*

Hosea 4:17,

> *Efraimu amejiunganisha na sanamu zake: mwache.*

Angalia hasa ya kwamba adhabu ya kuabudu sanamu ilikuwa ni kwamba jina la kabila hilo ilibidi lifutwe kutoka „chini ya mbingu." Kumbukumbu la Torati 29:20. Halisemi ya kwamba lingefutwa „mbinguni," lakini kutoka chini ya mbingu. Na hivyo ndivyo ilivyo hasa, kwa kuwa sasa Israeli wamerudi Palestina, na hivi karibuni Bwana atawatia muhuri 144,000 wa hao. Lakini kutokana na idadi hiyo Dani na Efraimu hawapo.

Ufunuo 7:4-8,

> *"Nikasikia hesabu yao wliotiwa muhuri katika KILA kabila la Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu.*
>
> *Wa kabila ya Yuda kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Reubeni kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Gadi kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Asheri kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Naftali kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Manase kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Simeoni kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kablia ya Lawi kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Isakari kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Zabuloni kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Yusufu kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Benyamini kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri waliotiwa muhuri.*

(Angalia, Dani na Efraimu hawapo).

Sasa pamoja na jambo hili angalia Dan. 12:1 ambayo inawaorodhesha hawa mia na arobaini na nne elfu wanaotiwa muhuri wakati wa ule muhuri waa sita na wakati wa ile Dhiki Kuu ama taabu ya Yakobo.

> *"Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako: na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo: na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja ATAKAYEONEKANA AMEANDIKWA KATIKA KITABU KILE."*

Hata hivyo, baada ya kipindi hiki cha dhiki, (wakati wa ule utawala wa miaka elfu,) kama ulivyoonekana na Ezekieli katika 48:1-8, na 22-29 tunaona makabila yamerudi mara nyingine tena katika utaratibu wa Kiungu. *Lakini, tangu wakati ule Efraimu na Dani walipojiunga na sanamu, walikufa, na makabila hayo hayatambuliwi tena. Sasa natambua ya kwamba tangu kule kuharibiwa kwa Yerusalemu, orodha zote za makabila yote zimepotea, hivi kwamba hakuna mtu anayeweza kusema kwa hakika yeye ni wa kabila gani, LAKINI MUNGU ANAJUA. Yale Mungu mkuu Ambaye anawarudisha Israeli Palestina anajua kwa uhakika kabisa kabila analotoka kila Mwisraeli halisi, na kutoka kwa hao wote mia na arobaini na nne elfu watakaookusanyika Dani na Efraimu hawatakuweko.*

Hapa kuna makabila ya Israeli. Ezekieli 48:1-8 na 22- 29,

> *"Basi, haya ndiyo majina ya kabila hizo. Toka mwisho wa pande za kaskazini, karibu na njia ya Hethloni hata maingilio ya Hamathi. Hata Hasar-enoni, penye mpaka wa Dameski, yaani, upande wa kaskazini karibu na Hamathi; watakuwa na upande wa mashariki na upande wa magharibi; Dani fungu moja.*
>
> *Tena mpakani mwake Dani, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, Asheri, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Asheri, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi; Naftali, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Naftali, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi; Manase, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Manase, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi; Efraimu, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Efraimu, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi; Reubeni, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Reubeni, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi; Yuda, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Yuda, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, nk.*
>
> *Tena tokea milki ya Walawi, na tokea milki ya mji, kwa kuwa ni katikati ya nchi iliyo ya mkuu katikati ya mpaka wa Yuda na mpaka wa Benyamini, itakuwa ya MKUU.*
>
> *Na katika habari za kabila zilizosalia; toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, Benyamini, fungu moja.*
>
> *Tena mpakani mwa Benyamini, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, Simeoni, fungu moja.*
>
> *Tena mpakani mwa Simeoni, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, Isakari, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Isakari, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, Zabuloni, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Zabuloni, toka upande wa mashariki hata upande wa magharibi, Gadi, fungu moja.*
>
> *Na mpakani mwa Gadi, upande wa kusini kuelekea kusini, nk.*

Mfano mwingine ambao tungeweza kuchukua ni habari za Israeli walipoondoka Misri wakielekea nchi ya Kanaani. Kusudi la Mungu katika wakati huu lilikuwa ni KUWATOA Israeli, na KUWAINGIZA, wapate kumtumikia Yeye. Hivyo basi wakati walipotoka Misri WOTE walitoka chini ya damu ya mwana-kondoo wa sadaka; WOTE walipitia ubatizo wa maji katika Bahari ya Shamu; WOTE waliifurahia miujiza yenye uwezo; WOTE walikula mana; WOTE waliunywea ule mwamba; na kwa habari za baraka dhahiri za nje na kuhusu madhihirisho WOTE walishiriki kwa njia ile ile na njia sawa. Lakini, walipofika Moabu wale waliojiunga na karamu ya Baal-Peori wote walikufa. Mizoga yao ilianguka nyikani, kwa sababu huko ndiko walikolikatalia

Neno la Mungu na wakaliacha. Sasa hili ndilo Ebr. 6:1-9 inachozungumzia, ambalo lilifafanuliwa vizuri sana katika Wakati wa Pergamo. Huwezi kuendelea na sehemu tu ya Neno, huna budi kuchukua Neno LOTE. Kuna watu wanaoonekana wanahusika na mambo ya Mungu karibu asilimia mia moja. Wao ni kama Yuda. Hakuna mtu ila Yesu aliyejua hasa Yuda alikuwa mtu wa aina gani. Kwa hiyo siku ikaja ambapo Yuda alifanya vile hasa Israeli walivyofanya huko Baali-peori. Alikata shauri ya kwamba alitaka kujiunga na jeshi la mzabibu wa uongo_ajiingize katika madhehebu ya biashara, na ya kisiasa yanayolipinga Neno, dini ya mpinga-Kristo na akafanya hivyo. Alidanganywa! Hao wengine kumi na mmoja hawakudanganyika. Hawangeweza kudanganywa, kwa maana walikuwa wateule wenyewe hasa. Kwa hiyo wakati Yuda alipoondoka na kumsaliti Bwana, jina lake liliondolewa kwenye Kitabu cha Uzima. (Ufunuo 22:19).

Sasa nina hakika ya kwamba umeona ya kwamba hao ambao majina yao yalikuwa katika Kitabu cha Uzima walikuwa ni sehemu ya utaratibu wa dini wa siku hizo uliokuwa unaegemea kwa Mungu wa kweli na kumwabudu Yeye, ingawa hawakuabudu kulingana na Kweli (Neno.) Kama vile Yuda wao hawakuendelea hata mwisho. Angalia jinsi Yuda alivyochaguliwa na Mungu. Yeye alifundishwa katika kweli. Yeye alishiriki maarifa ya siri. Alipewa huduma yenye nguvu na aliwaponya wagonjwa na kutoa pepo katika Jina la Yesu. Lakini wakati shindano la kuamua lilipokuja, yeye alijiuza kwa dhahabu na nguvu za kisiasa. Yeye hakufika Pentekoste kumpokea Roho wa Mungu. Hakuwa na Roho. Usikosee, mtu ambaye amebatizwa kweli na Roho Mtakatifu katika mwili wa Kristo na kupokea utimilifu wa Roho atakuwa katika NENO DAIMA. Hilo ndilo thibitisho la kubatizwa na Roho Mtakatifu. Yuda alishindwa. Umati wa watu unashindwa papo hapo. Na wakati wanaposhindwa kuendelea katika Neno hilo, majina yao yanaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima.

Ili kufafanua zaidi kuondolewa huku kwa jina kutoka katika Kitabu cha Uzima tunapaswa kupanua mawazo yetu kwa Israeli katika siku za Musa.

Kutoka 32:30-34,

> *"Hata asubuhi yake Musa akawaambia watu, Mmetenda dhambi kuu: na sasa nitakwenda juu kwa Bwana; labda nitafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zenu.*
>
> *Musa akarejea kwa Bwana, akasema, Aa! watu hawa wametenda dhambi kuu, wamejifanyia miungu ya dhahabu.*
>
> *Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi zao—, na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu Chako ulichokiandika.*
>
> *Bwana akamwambia Musa, Mtu ye yote aliyenitenda dhambi, ndiye nitakayemfuta katika kitabu Changu.*
>
> *Basi sasa uende ukawaongoze watu hawa mpaka mahali pale ambapo nimekuambia habari zake; tazama, malaika Wangu atakutangulia; pamoja na hayo siku nitakayowajilia nitawapatiliza kwa ajili ya dhambi yao.*

Ni dhahiri kweli kweli ya kwamba majina yameondolewa, na yataondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima kabla ya wakati haujaisha. Katika mahali hapa hasa ilikuwa ni kwa sababu ya kuabudu sanamu, kama vile Dani na Efraimu walivyopoteza haki zao kama makabila kwa ajili ya kuabudu ndama za dhahabu. Wote walioabudu sanamu majina yao yaliondolewa katika Kitabu cha Uzima.

Wakati Israeli walipoukataa uongozi wa Mungu katika nguzo ya moto, na kugeukia ibada za ndama wa dhahabu majina yao yaliondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima. Kutoka 32:33. *(Mtu ye yote aliyenitenda dhambi, ndiye nitakayemfuta katika kitabu Changu.)* Kama kugeukia sanamu namna hiyo kunastahili adhabu ya majina kuondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima, basi bila shaka kabisa Israeli kumkataa Yesu Kristo kama Masihi kungestahili adhabu kali kama hiyo. Hivi ndivyo ilivyo hasa.

Katika Zaburi 69 ambayo inaelezea kutwezwa kwa Yesu inasema katika aya ya 21-28,

> *"Wakanipa uchungu kuwa chakula Changu; Nami nilipokuwa na kiu wakaninywesha siki.*
>
> *Meza yao mbele yao na iwe mtego; naam, wakiwa salama na iwe tanzi.*
>
> *Macho yao yatiwe giza wasione, na viuno vyao uvitetemeshe daima.*
>
> *Uimwage ghadhabu Yako juu yao, na ukali wa hasira Yako uwapate.*
>
> *Matuo yao na yawe ukiwa: pasiwe na mtu wa kukaa hemani mwao.*
>
> *Maana wanamwudhi Mtu uliyempiga Wewe, wanasimulia maumivu ya hao uliowatia jeraha.*
>
> *Uwaongezee uovu juu ya uovu, wala wasiingie katika haki Yako.*

*Na wafutwe katika Chuo cha Uhai, wala pamoja na wenye haki wasiandikwe."*

Wakati Wayahudi walipomkataa Yesu Mungu aliwaacha kweli akawaendea Mataifa.

Matendo 13:46-48,

*"Paulo na Barnaba wakanena kwa ushujaa wakasema, Ilikuwa lazima Neno la Mungu linenwe kwenu kwanza; lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele, angalieni, twawageukia Mataifa.*

*Kwa sababu ndivyo tulivyoamriwa na Bwana, akinena, Nimekuweka uwe nuru ya Mataifa, upate kuwa wokovu hata mwisho wa dunia.*

*Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza Neno la Bwana: nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini."*

Hii si kudokeza ya kwamba hakutakuweko na majina mengine tena kutoka katika makabila ya Israeli yatakayosalia katika Kitabu cha Uzima, kwa maana wengi wa hawa (bali si umati wa watu) kwa kanuni ya kuteuliwa watakuwa katika wakati wa kanisa la Mataifa na kuingia katika mwili wa Yesu Kristo, ikionyesha ya kwamba majina yao kweli yalibaki katika Kitabu cha Uzima. Pia, kama tutakavyoonyesha, kulingana na muhuri ya sita umati mkubwa wa mashahidi wa Kiyahudi watapewa mavazi meupe na uzima wa milele na Bwana. Pia wale mia na arobaini na nne elfu watatiwa muhuri wakati wa kule kuja Kwake, ikithibitisha ya kwamba majina yao hayakufutwa pia. Lakini ni kama tu ilivyoelezwa kwa usahihi sana katika Zaburi ya 69 ya kwamba ni hao waovu ama watu wasio na haki wanaomkataa Kristo na wanaowaangamiza watu Wake ambao majina yao yanaondolewa.

Kama vile Israeli (watu waliochaguliwa na Mungu) walio wengi walivyopoteza haki zao katika Kitabu cha Uzima kwa kumkataa Yesu, vivyo hivyo wengi wa kanisa la Mataifa watahukumiwa pia na matokeo yake yatakuwa kuondolewa kwa majina yao kutoka katika Kitabu cha Uzima kwa kulikataa Neno na hivyo basi kuingia katika harakati za ekumeni ulimwenguni kitu ambacho ni sanamu iliyotengenezwa kwa ajili ya yule mnyama.

Kuna jambo lingine la kuona hapa. Katika ile hukumu kuu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi kutakuweko na watu kubaguliwa. Kitabu cha Uzima kitafunguliwa na kitabu kingine kitafunguliwa.

Mathayo 25:31-46,

*"Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu Wake;*

*Na mataifa yote watakusanyika mbele Zake; Naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi;*

*Atawaweka kondoo mkono Wake wa kuume, na mbuzi mkono Wake wa kushoto.*

*Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono Wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu:*

*Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula: Nalikuwa na kiu, mkaninywesha; Nalikuwa mgeni, mkanikaribisha:*

*Nalikuwa uchi, mkanivika: Nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama: nalikuwa kifungoni, mkanijia:*

*Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha;*

*Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha? au u uchi, tukakuvika?*

*Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia?*

*Na Mfalme atajibu akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi.*

*Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari ibilisi na malaika zake.*

*Kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula: Nalikuwa na kiu, msininyweshe:*

*Nalikuwa mgeni, msinikaribishe: nalikuwa uchi, msinivike: Nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama:*

*Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona Wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie?*

*Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi.*

*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele."*

Ufunuo 20:11-15,

*"Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na Yeye aketiye juu yake; Ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso Wake, na mahali pao hapakuonekana.*

*Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele za Mungu; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni Kitabu cha Uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao,*

*Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake: na mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.*

*Mauti na kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili.*

*Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika Kitabu cha Uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."*

Kutakuwako na wenye haki na wasio haki pia katika hukumu hii. Inasema hivyo. WENYE HAKI HAWA HAWATAKUWA BIBI- ARUSI KWA MAANA BIBI-ARUSI ANAKETI NAYE KATIKA HUKUMU.

I Wakorintho 6:2-3,

*"Au hamjui ya kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu? na ikiwa ulimwengu utahukumiwa na ninyi, je! hamstahili kukata hukumu zilizo ndogo?*

*Hamjui ya kuwa tutawahukumu malaika? basi si zaidi sana mambo ya maisha haya?*

Ufunuo 3:21,

*"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi."*

Mnaona, Bibi-arusi yuko pamoja Naye kwenye kile kiti cha enzi. Kwa kuwa yeye atauhukumu ulimwengu hana budi kuketi katika hukumu pamoja Naye. Hayo ndiyo hasa aliyoona Danieli.

Danieli 7:9-10,

*"Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi Yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa Chake kama sufu safi: kiti Chake cha enzi kilikuwa kama miali ya moto, na gurudumu Zake kama moto uwakao.*

*Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele Zake: maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele Zake: hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa."*

Mnaona, ni tukio lile lile, kwa maana wale maelfu mara elfu wanaomtumikia Yeye ni bibi-arusi, kwa kuwa ni nani anayemtumikia mume isipokuwa mke?

Swali sasa linazuka, kwa nini hawa wenye haki wawe katika hukumu? Hakuna mahali pengine wanapoweza kutokea, kwa maana kuna ufufuo mara mbili tu na kwa kuwa hawangeweza kustahili ufufuo wa kwanza hawana budi kutokea katika wa pili ambao ni ufufuo wa hukumu. Wale wanaostahili ufufuo wa kwanza (bibi-arusi) hawako hukumuni. Yohana 5:24, *"Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele (hiyo ni kusema, mwamini tayari amepokea uzima wa milele ambao anao sasa kama mali yake); wala hataingia hukumuni (hataingia hukumuni, ndivyo inavyosema hasa) bali amepita (daima) kutoka mautini kuingia uzimani."* Lakini angalia kwa makini, Yesu hana budi analiwazia kundi lingine bado ambalo katika ufufuo fulani litapokea uzima wa milele. Wao wataupokea kwenye ule ufufuo, KWA KUWA HAWAKUWA WAMEUPOKEA HAPO AWALI KAMA SEHEMU YA BIBI-ARUSI.

Yohana 5:28- 29,

*"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu WOTE waliomo makaburini wataisikia sauti Yake,*

*Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu."*

Sasa sote tunajua ya kwamba Yn. 5:28-29 SI KULE KUNYAKULIWA kwa kuwa ni wale tu waliokufa katika Kristo watakaofufuka kutoka makaburini wakati huo pamoja na bibi-arusi ambaye angali hai duniani.

I Wathesalonike 4:16-17,

*"Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.*

*Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele."*

Lakini inasema katika Yn. 5:28-29 ya kwamba WOTE watatoka kaburini. Huu ni ufufuo ule ule unaonenwa katika Ufu. 20:11- 15 ambapo WALIOKUFA waliletwa mbele za Bwana na kuhukumiwa kulingana na kazi zao, na wote wale ambao majina yao hayakuwemo katika Kitabu cha Uzima basi walitupwa katika lile ziwa la moto.

Sasa tunalikabili swali kwamba ni kwa sababu gani wanapaswa kupewa uzima wa milele kwenye ile hukumu kwa sababu inaonekana Nyaraka zinaonekana zinasisitiza kinaganaga ya kwamba mtu hana budi kuwa na Roho wa Kristo la sivyo ataangamia. Ingawa inaonekana hivi, hatupaswi kuyapuuza maneno ya Yesu Ambaye anasisitiza ya kwamba kuna wengine wanaopatikana katika Kitabu cha Uzima ambao aidha watapokea uzima wa milele kabla ya ufufuo wa kiama ama baada yake.

Paulo haepi kweli hii kwa sababu yeye anasema kwa udhahiri sana katika Flp. 3:11,

*"Ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiama ya wafu."*

Sasa tamshi hili ni la kipekee sana. Sote tunajua ya kwamba sisi SOTE tutafufuka tutake tusitake. Wote watafufuliwa. Kwa hiyo hata kidogo kwamba Paulo asingeweza kuwa anasema, "Ili KWA NJIA YO YOTE nipate kuifikia kiama ya wafu." Ukweli wa mambo ni kwamba, yeye hasemi hivyo. Maana hasa ya maneno hayo ni kwamba, "Ili kwa njia yo yote nipate kufikia „kufufuka nje ya kiama" ya wafu." Hii si kufikia kiama ya watu wote ama ufufuo wa pili, lakini ni kufikia ufufuo wa kwanza, ambao habari zake zinasemwa, "Heri na Mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza, juu ya hao mauti ya pili haina nguvu, bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo nao watatawala pamoja Naye hiyo miaka elfu." Ufufuo wa kwanza hauna uhusiano wo wote na mauti ya pili. Huo ni mwisho wa ile miaka elfu wakati HAO wafu WALIOSALIA watakuwa tena hai. Na katika siku hiyo kutakuweko na hao watakaotoka waingie uzima wa milele na wale wengine watakaopatikana na mauti ya pili. Sasa hatutaki kubahatisha kuhusu wale ambao watakaopewa uzima katika ule ufufuo wa pili. Tunaambiwa wanapewa uzima kwa kuwa wamekuwa wema na wakarimu kwa "Ndugu." Wale watakaofufuliwa na kutupwa kwenye lile ziwa la moto watatendewa hayo kwa sababu ya kuwatendea mabaya "Ndugu." Kwa kuwa hili ni Neno la Mungu tunalikubali kirahisi tu. Hakuna hoja hapa, tamshi rahisi tu la ukweli.

Ili kufafanua zaidi, angalia hasa maneno ya Mathayo 25:31-46. Halisemi ya kwamba mchungaji kwa kweli anawatenganisha kondoo na mbuzi, bali ni kama mchungaji anayewagawanya kondoo na mbuzi. Hawa si kondoo katika muda huu maalum (Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi). Kondoo wamo zizini Mwake, waliisikia sauti Yake (Neno) nao wakamfuata. TAYARI WANA UZIMA WA MILELE WALA HAWAWEZI KUINGIA HUKUMUNI. Lakini hawa HAWANA uzima wa milele, nao wako hukumuni. Wanaruhusiwa kuingia katika uzima wa milele. Lakini wanaingia katika uzima wa milele kwa masharti gani? Bila shaka si juu ya jambo kwamba wao tayari wana uzima Wake kama vile bibi-arusi alivyo nao, lakini wanaupokea kwa sababu waliwatendea mema ndugu Zake. Wao si ndugu Zake; hilo lingewafanya warithi pamoja na Yesu. SI warithi wa cho chote ila uzima. Hawashiriki kiti cha enzi, na kadhalika pamoja Naye. MAJINA YAO HAPANA BUDI YALIKUWA KWENYE KITABU CHA UZIMA WALA HAYAKUONDOLEWA. Sasa kwa sababu ya upendo wao kwa watu wa Mungu wanatambuliwa na kuokolewa. Hapana shaka hawa waliwahudumia na kuwasaidia watoto wa Mungu. Labda kama akina Nikodemu na Gamalieli waliwatetea watoto wa Mungu katika wakati wa shida.

Kama hili linaonekana linafanana na "kurudishwa," angalia kwa makini sasa, kwa maana walio waovu Hawarudishwi, lakini wanatupwa kwenye lile ziwa la moto. Majina ya wengi wa wale wanaoangamizwa yalikuwa katika kile Kitabu cha Uzima pia; lakini yalifutwa kwa sababu walishindwa kuwaheshimu watu wa Mungu waliokuwa Neno lililo hai lililodhihirishwa (nyaraka zilizo hai) kwa siku yao.

Sasa hebu na tuwe wazi sana hapa. Haya si mataifa yanayohukumiwa na kuingia katika ule utawala wa miaka elfu ati kwa sababu wamewakaribisha na kuwasaidia Wayahudi. Hilo ni wazi sana kwa sababu ya mwisho wa aya hizi. *"Basi hawa (waovu) wataingia katika adhabu ya milele (ziwa la moto), lakini wenye haki katika uzima wa milele."* Hakuna kumbukumbu ya hukumu mbili zilizowekwa ambapo waovu wanatupwa katika ziwa la moto. Ni mnyama tu na nabii wa uongo wanahukumiwa mwisho wa ile dhiki

kuu. La, hii ni hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi, nao wanahukumiwa kulingana na yale yaliyoandikwa katika vitabu.

Ni katika ufufuo wa pili ambapo zile "roho zilizo chini ya madhabahu" kama ilivyoelezewa katika muhuri ya tano (Ufu. 6:9-11) wanaopewa nguo ndefu nyeupe, na hakuna budi uzima wa milele, la sivyo kusingekuwa na haja ya nguo ndefu nyeupe.

> *"Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya Neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.*
>
> *Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Mola, Mtakatifu, Mwenye kweli, hata lini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?*
>
> *Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao."*

Sasa angalia hasa ya kwamba hakuna mmoja wa hawa walio chini ya madhabahu waliuawa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu. Hawakuwa kama Antipa aliyeuawa kwa kushikilia sana Jina Lake. Hawa hawajazaliwa mara ya pili, wakiwa na uhai wa milele kama milki yao. Wanakuja katika ufufuo na kupokea uzima kwa sababu ya msimamo wao juu ya Neno. Na angalia jinsi hawa wanavyolilia kulipiziwa kisasi. Hawawezi kuwa ni ule mwili wa bibi-arusi. Bibi-arusi hugeuza shavu na kupaza sauti, "Wasamehe, Baba, hawajui watendalo." Hawa ni Wayahudi. Hawana budi kuwa kwa sababu wako kwenye muhuri ya tano, na ni katika muhuri ya nne ambapo bibi-arusi wa Mataifa ananyakuliwa. Kwa hiyo Wayahudi hawa hawakuzaliwa kwa Roho Wake. Hata hawaamini ya kwamba Yesu ni Masihi. Lakini kwa kuwa walipofushwa na Mungu kwa ajili ya Mataifa, Mungu aliwapa uzima wa milele kwa sababu kwamba ingawa hawangeweza kuja Kwake, hata hivyo walikuwa waaminifu kweli kwa Neno lote walilojua, na wakalifia kama vile umati mkubwa ulivyokufa chini ya Hitla, Stalin, nk. na bado watakufa.

Ni ufufuo wa pili ambapo wale wanawali watano wapumbavu walitokea. Angalia ya kwamba wao walikuwa wanawali. Hawakuwa na Roho Mtakatifu kwa hiyo walikosa kuwa katika bibi-arusi, wakati wale wenye busara watano waliokuwa na mafuta wakawa sehemu ya huyo bibi-arusi. Lakini watu hawa, wakiwa ni watu waliotengwa, wanaompenda Mungu, na wakijaribu kukaa katika Neno, kulingana na walivyojua jambo hilo, na wakiwa msaada katika kazi ya Bwana watakuja mwishoni mwa wakati. Watakosa kuweko kwenye ule utawala wa miaka elfu, ambao unaweza kuanza kuona kulingana na kweli hizi kuwa ni muhimu zaidi na mzuri mno kuliko tulivyoweza kuwazia ama kuamini.

Watu hawa wote majina yao yalikuwa katika Kitabu cha Uzima na majina yao yalibakia. Lakini ni akina nani ambao hawakusalia? Wale wa makanisa ya mfumo wa ulimwengu waliopigana na bibi-arusi watakuwa ndio ambao majina yao yanaondolewa. Hao ndio watakaoshindwa. Watatupwa katika ziwa la moto.

Sasa hebu na tuchukue hatua nyingine, lakini kabla hatujafanya hivyo na tupitie kesi yetu mpaka sasa. Kwanza kabisa tunajua hakika kabisa kwamba kusudi la Mungu linasimama katika kuchaguliwa. Ilikusudiwa ndani Yake Mwenyewe. Lilikuwa ni kusudi la Mungu kuwaleta watu kama Yeye ambao wangekuwa Bibi-arusi Neno. Yeye alichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu KATIKA YEYE. Yeye alijulikana sana na kupendwa kabla hajazaliwa katika zile nyakati juu ya nchi. Alikuwa amekombolewa kwa damu Yake na hawezi kamwe kuingia katika hukumu. Hawezi kamwe kuwa hukumuni kwa sababu dhambi haiwezi kuhesabiwa kwake.

Warumi 4:8,

> *"Heri mtu yule ambaye Bwana hatamhesabia dhambi."*

Lakini hakika yeye atakuwa pamoja Naye katika kiti Chake cha hukumu, akiuhukumu ulimwengu na hata malaika. Jina lake (kila mmoja wa washiriki wake) liliandikwa katika sehemu ya Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Pili, kuna tabaka lingine. Majina yao pia yako katika Kitabu cha Uzima na watafufuka katika ufufuo wa pili. Hao ndio wanawali wapumbavu na wenye haki kama inavyonenwa katika Mathayo 25. Katika tabaka hili pia kuna wale wasiomwabudu mnyama wala kuhusika katika mfumo wa mpinga-Kristo bali wanakufa kwa ajili ya imani yao ingawa hawako katika bibi-arusi, hawajazaliwa mara ya pili. Lakini watafufuka katika ufufuo wa pili na kuingia katika uzima wa milele. Tatu, kuna Wakristo wakwamia mpakani kama tulivyoona katika Israeli wakitoka Misri. Hawa walikuwa na majina yao katika Kitabu cha Uzima na kazi zao zimeandikwa katika vitabu hivyo. Watu hawa baada ya kushindwa kumtii Mungu na wakiwa hawana Roho, ingawa hata ishara na maajabu yalikuwa miongoni mwao, majina yao yataondolewa kwenye Kitabu cha Uzima. Kati ya kundi hili kutakuweko na wale kama Yuda ambao ingawa hawana Roho kabisa, lakini ni wa kidini, watakuwa na madhihirisho maishani mwao, na ingawa walikuwa kwenye vile vitabu hawakuwa wamechaguliwa KATIKA YEYE. Watu pia kama Balaamu watakuwa kwenye kundi hilo. Nne na mwisho ni wale ambao majina yao hayajapata kuandikwa wala hayataandikwa katika vile vitabu.

Watu kama hao wanapatikana katika Ufu. 13:8 na Ufu. 17:8,

> *"Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana- Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.*
>
> *Yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi wasioandikwa majina yao katika Kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako."*

Yesu alisema ya kwamba kundi fulani lingemkubali mtu aliyekuja kwa jina lake mwenyewe. Huyo ni mpinga-Kristo. Na hivyo ndivyo hasa inavyosema juu yao katika Ufunuo 13:8, na 17:8. Hawa waliamriwa na Mungu bali si kwa ajili ya kuteuliwa. Na pamoja na kundi hili wapo walio kama Farao.

Inasema juu yake,

> *"Nilikusimamisha kwa kusudi hili, ili nionyeshe nguvu Zangu kwako. Vyombo vya ghadhabu vilivyofanywa tayari kwa uharibifu."*

Warumi 9:17 na 22.

Hakuna mmoja wa hawa angewekwa kwenye zile orodha za uzima. Sisemi ya kwamba hakuna orodha yao. Hapana shaka kuna namna fulani ya orodha yao, lakini SI KATIKA ILE ORODHA YA UZIMA. Kusudi la kuwepo kwao limegusiwa kidogo katika sehemu iliyobaki ya kitabu hiki lakini tunaweza kuongezea Maandiko mengine mawili.

Mithali 16:4,

> *"Bwana amewafanya wabaya kwa siku ya ubaya."*

Ayubu 21:30,

> *"Mwovu huachiliwa katika siku ya msiba, na kuongozwa nje katika siku ya ghadhabu."*

Kwa kuwa sehemu hii ya Neno ni ngumu kwa akili ya mwanadamu kufahamu, haina budi kukubaliwa na kuaminiwa kwa imani. Wengine watachukizwa na yale niliyoeleza kwa sababu wanashindwa kufahamu uwezo mkuu wa Mungu ambao hutangaza kwamba MUNGU NI MUNGU, na kwa kuwa Yeye ni Mungu mtu hawezi kushinda mashauri Yake wala kuzuia mapenzi Yake na kusudi Lake; lakini Yeye, akiwa ni mwenye nguvu zote, anatawala katika mambo YOTE na anafanya lo lote atakalo na viumbe vyake vyote kwa sababu vyote viliumbwa kwa ajili ya mapenzi Yake mema. Kwa hiyo, kama Paulo asemavyo, "Kama Mungu akichukua fungu moja la udongo na kufanya kutoka kwenye fungu lilo hilo chombo kimoja cha heshima na chombo kingine cha ghadhabu Yake, ni nani anayeweza kuchukizwa Naye na kumpigia makelele?" Kwamba Yeye ana haki ya kufanya jambo hili kwa misingi ya uumbaji peke yake, hatuwezi kukana. Hata hivyo alienda hata mbele zaidi, kwa maana kulingana na Rum. 14:7-9, tuna thibitisho lisiloweza kukanushwa ya kwamba Yesu alilipa gharama ya ulimwengu mzima, na kwa hiyo anaweza kufanya apendavyo na walio Wake.

> *"Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake.*
>
> *Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana, au kama tukifa, twafa kwa Bwana: basi kama tukiishi au kama tukifa, tu mali ya Bwana*
>
> *Maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, AWAMILIKI WALIOKUFA NA WALIO HAI PIA."*

(Ni kumiliki: SI uhusiano unaomaanishwa hapa.)

Hii pia imewekwa katika Yohana 17:2,

> *"Kama vile ulivyompa mamlaka JUU YA WOTE WENYE MWILI, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele."*

Sasa, kama tukimpa Mungu sifa ya kujua yote, hatuna budi kukubali pia ya kwamba Yeye ni mkamilifu katika hekima na haki. Mpango huu wa kuchagua na kukatalia ni hekima ya Mungu iliyofunuliwa katika nyakati zote yaani, kama vile isemavyo katika Efe. 1:3-11,

> *"Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za Rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani Yake Kristo;*
>
> Kama vile alivyotuchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele Zake katika pendo.*

*Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake.*

*Na usifiwe utukufu wa neema Yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa.*

*Katika Yeye huyo, kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake.*

*Naye alituzidishia hiyo katika HEKIMA yote na ujuzi,*

Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi Yake, sawasawa na uradhi Wake, alioukusudia katika Yeye huyo.*

*Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia.*

*Naam, katika Yeye huyo; na ndani Yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi Lake Yeye, Ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi Yake."*

Kwa hiyo kama Mungu ameamua kwamba kuweko na hao ambao majina yao yanawekwa katika sehemu fulani ya Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo na hayawezi yakafutwa kwa maana ni majina ya bibi-arusi Wake, basi hatuna budi kukubali hilo. Kama inasemwa pia kwamba kuna wale ambao majina yao yaliwekwa katika orodha ya Kitabu cha Uzima lakini katika kutangulia kujua kwa Mungu ilikuwa waanguke na kuondolewa majina yao hatuna budi kukubali jambo hilo. Na kama kuna hao ambao majina yao KAMWE hayakuandikwa kwenye orodha ya uzima, hatuna budi kukubali jambo hilo, pia. Na kama kuna hao ambao wataingia katika uzima wa milele baada ya ile hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi kwa sababu tu waliwatendea mema na kuwafadhili na kuwapa haki yao wateule wa Mungu ambao ni ndugu Zake, basi hatuwezi ila kukubali jambo hilo. MAANA NI NANI ALIYEIFAHAMU NIA YA BWANA AMWELIMISHE? Badala yake hebu na tuwe watiifu katika imani kwa Yeye Ambaye ni Baba Yetu tupate kuishi.

Ili kufahamu somo hili yaani kwa dhahiri sana itakuwa vema kuliendea sasa kutokana na wazo la kanisa katika zile nyakati zote. Mpaka wakati huu tumekuwa tukifikiria juu ya kuondolewa kwa majina ya watu binafsi. Sasa tunataka kufikiria, si watu binafsi, bali makundi yaliyowakilishwa kanisani. Kufanya hivyo tutalifananisha kanisa katika nyakati zote na mmea wa ngano. Punje ya ngano inapandwa ili kwamba punje moja ya ngano itazaa na kuongezeka kupitia hatua fulani katika muda fulani wa wakati. Hiyo punje moja itakufa, lakini katika kufa, uhai ule uliokuwemo ndani yake utapanda juu katika mmea ambao nao utakuwa mbebaji ama mchukuzi wa uhai huo ambao hauna budi kurudia hali ya asili katika hali ya wingi. Yesu Mzao mkuu wa Kifalme alikufa. Huyo Mwenyezi Ambaye ndiye uzima wa kanisa anasimama katikati ya kanisa kwa zile nyakati saba zote za kanisa akitoa uhai Wake kwa kanisa (bebaji ama chukuzi) ili kwamba uhai Wake wenyewe utazaliwa tena katika miili inayofanana na Wake katika ule ufufuo. Katika wakati ule wa ufufuo ndipo ambapo ule Mzao wa Kifalme utaona mizao mingi ya kifalme ifananayo na Yeye Mwenyewe, nao hata watakuwa kama alivyo Yeye, kwa kuwa Yohana anasema, "tutakuwa kama Yeye." Jambo hili ndilo ambalo Yohana Mbatizaji alilokuwa akilinena aliposema kwamba Yesu angekusanya ngano ghalani. Huo ulikuwa ni ule ufufuo ambapo wale waliokombolewa waliokuwa wamechaguliwa kupata uzima wa milele walipoingilia.

Sasa basi, orodha ya mmea huu wa ngano ambao mwisho wake ni kuzaa tena ile mbegu ya asili katika mbegu nyingi ndicho KITABU CHA UZIMA. Narudia: historia ama orodha ya mmea huu wa ngano ni Kitabu cha Uzima ambacho sehemu ya Kitabu kile cha Uzima ni ORODHA YA UZIMA WA MILELE. (Sehemu fulani ya Kitabu cha Uzima). Jambo hili linakuwa dhahiri kwa kuchunguza mmea wa ngano. Mbegu tupu hupandwa. Mara jani linatokeza. Lakini hiyo si ngano bado. Ndipo inakua shina. Hii bado si ngano. Uhai upo, bali si ngano. Ndipo kwenye mwisho wa ule ubua kuna kitu kilichochongoka kinachotoa kishada. Bado ni mmea wa ngano lakini ngano yenyewe bado. Kisha huo mmea unapata mbelewele, ndipo tunaona kapi likitokea. Hili linafanana sana na ngano lakini bado si mbegu. Halafu inaunda ngano katika ganda. Sasa imerudi kwenye kile ilichokuwa hapo awali. Sasa ngano iliyoiva imevunwa.

Yesu Kristo alikufa. Yeye alitoa uhai Wake. Uhai huo ulikuwa urudi juu ya kanisa na kuwaleta wana wengi kama Yeye kwa utukufu katika ufufuo. Lakini kama vile ile punje ya ngano ilivyopaswa kuwa na mbebaji kusudi izae punje nyingi za ngano, hata hivyo kulipaswa kuwe na kanisa ambalo lingekuwa bebaji la Uzima wa Kristo. Kama vile ule unyasi, ubua, kishada, na maganda yalivyokuwa wabebaji wa ile mbegu lakini HAYAKUWA ile mbegu yenyewe, vivyo hivyo kanisa lote katika nyakati zote limekuwa bebaji la MBEGU ya kweli ingawa lenyewe SI mbegu. Hiyo ndiyo sababu tunaweza kusema ya kwamba Kitabu cha Uzima ni mmea MZIMA WA NGANO.

Hebu na turudie hilo tena. Hii hapa ile mbegu asili ambayo ilipandwa. Ilitoa jani. Hilo halikuwa mbegu. Ikatoa ubua. Huo si yenyewe. Haya hapa maganda ambamo ngano itaumbika. Hayo siyo. Kishada kinatokea. KISHA MBELEWELE ZINAANGUKIA ZILE SEHEMU ZA MBEGU. SEHEMU YA MMEA HUO

INAHUISHWA. KITU FULANI CHA ILE MBEGU ASILI KILICHOPANDA KUPITIA KWENYE MMEA WOTE KINAGEUKA KIKAWA MBEGU. Kwa nini mmea wote haukugeuka ukawa mbegu? Kwa sababu uliumbwa kwa kusudi hilo. Ni sehmu tu ya mmea huo inayoweza kurudi ikawa mbegu kwa sababu ni sehemu tu ya MMEA huo wa NGANO NDIYO NGANO YA UZIMA WA MILELE.

Mna mfano mkamilifu wa hilo katika Israeli wakiondoka Misri. Walitoka kama watu milioni mbili wenye nguvu. WOTE waliokoka kupitia damu ya dhabihu. WOTE walibatizwa katika Bahari ya Shamu; WOTE walitoka majini wakifurahia dhihirisho la Roho Mtakatifu na baraka; WOTE walikula chakula cha malaika; WOTE waliunywea ule mwamba uliowafuata. Hata hivyo ila kwa wachache sana hawakuwa kitu ila wabebaji kwa ajili ya watoto ambao wangewafuata na kuingia katika nchi ya Kanaani. Israeli wote SI Israeli. Na wote ila ukiondoa watu wachache sana majina yao yalifutwa kutoka katika Kitabu cha Uzima.

Tuna haki ile ile leo kanisani. Majina yatafutwa kwenye Kitabu cha Uzima. Hakuna jina litakaloondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima wa Milele kwa maana hiyo ni orodha nyingine ikiwa iko kwenye Kitabu cha Uzima. HUU NDIO USHUHUDA: MUNGU AMETUPA UZIMA WA MILELE, NA UZIMA HUU UMO KATIKA MWANAWE. YEYE ALIYE NAYE MWANA ANAO HUO UZIMA (WA MILELE) ASIYE NAYE MWANA HANA HUO UZIMA (WA MILELE). Na hao walio na huo uzima walikuwa katika YEYE kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. WALICHAGULIWA KATIKA YEYE KABLA YA KUWEKWA MISINGI YA ULIMWENGU. Huo MZAO MKUU WA KIFALME, Yesu Kristo, alipandwa (alikufa) na uhai huo uliokuwemo ndani Yake ukapanda kupitia katika mmea wa ngano na unajizaa wenyewe katika punje nyingi za ngano zilizo na uzima ule ule ndani yao, na zikiwa kama ile ya Asili kwa sababu kwa njia ya Roho wao ni wa asili.

Sasa tunaweza kuona kwa nini bibi-arusi (alikuwa ndani Yake kama vile Hawa alivyokuwa ndani ya Adamu) aliyekombolewa (kununuliwa na kurudishwa na mwenyewe wa asili) hawezi kamwe kufutwa „majina ya washirika wake" kutoka kwenye ile orodha. Yeye ni sehemu Yake. Yeye yuko kwenye kiti cha enzi. Hawezi kamwe kuhukumiwa. Kila mmoja katika bibi-arusi ni mshirika Wake na Yeye hatampoteza hata mmoja. Lakini sivyo ilivyo kuhusu wale "wote" walio kwenye kile Kitabu cha Uzima. Kwa maana kati yao wako wale kama Yuda nk. walio na sehemu fulani katika ile orodha lakini majina yao yanaondolewa. Tunaweza kuona wale wanaokuja katika siku za mwisho, na baada ya kufanya matendo ya ajabu sana, Yesu atasema ya kwamba Yeye hakuwajua kamwe. Si kwamba hakuwa akijua wapo. Kujua Kwake mambo yote kunaliondoa jambo hilo; lakini wao hawakujulikana tangu zamani kama vile katika bibi-arusi; na wala hawakujulikana tangu zamani kama walio kati ya wenye haki wa ufufuo wa pili. Hawakuzaa matunda yo yote (kwa sababu walikuwa nje ya Neno_hawakudumu ndani ya Hilo) na wao, kwa sababu hii, walipewa adhabu ya kifo. Basi kama tulivyoonyesha hapo kabla kuna wale waliomtetea bibi-arusi na walikuwa msaada na faraja kwake. Hao majina yao yalibakia katika Kitabu cha Uzima na wanaingia katika uzima wa milele. Hatimaye kuna wale kama Farao ambao hawakuandikwa majina yao katika Kitabu cha Uzima na hawa wanatupwa katika ziwa la moto pia.

Hivyo basi punje ile ya ngano iliyokuwa mmea wa kuvunwa ni kumbukumbu za kanisa. Na kama vile ambavyo mmea wote wa ngano sio ngano yenyewe, na kama vile ambavyo si mmea wote unaotumiwa katika mavuno, ndivyo iliyo na kanisa:_kanisa lote si bibi-arusi, na wala si wote wanaopewa uzima wa milele, lakini SEHEMU yake inakusanywa katika ghala, na SEHEMU yake inawekwa ili kwamba ipate kuingia katika uzima wa milele katika ufufuo wa pili, na SEHEMU yake ambayo inahesabiwa kama kapi inachomwa katika lile ziwa la moto.

Na jambo hili ndilo hasa Yohana Mbatizaji pamoja na Yesu walilosema, kwa kuwa Yohana alisema ya kwamba ngano ingewekwa ghalani na makapi yachomwe moto. Yesu alisema, "Yafungeni magugu, kisha muikusanye ngano." Harakati za ekumeni zitayafunga pamoja makanisa magugu, kwa maana magugu hayana budi kufungwa KWANZA, na ingawa mwisho wao ni kuchomwa moto, hayachomwi wakati yanapofungwa lakini yanawekwa hadi wakati mwingine, ambao ni mwisho wa ule utawala wa miaka elfu, ama ufufuo wa pili. Lakini mara magugu yanapofungwa kunyakuliwa kunaweza kutokea na kunatokea wakati fulani kati ya kule kufungwa na kule kufunuliwa kwa mpinga-Kristo. Ndipo itakuja siku ambapo WOTE watasimama pamoja kama inavyoonekana katika Danieli. Mfalme atakuwa pale pamoja na bibi-arusi Wake na mbele yao kutakuwako na umati utakaohukumiwa. Ndiyo. Wote wako pale. Vitabu vyote vimefunguliwa. Mwelekeo wa mwisho wa watu WOTE unafanywa. Kuvuna kweli kumekwisha. Mara vitabu vikiisha kufunguliwa vinafungwa.

Katika kumalizia somo hili kwa wakati huu, hebu nirejee kwenye tamshi moja lililotolewa mwanzoni mwake ambapo nilisema ya kwamba hakuna hata Andiko moja linalonena juu ya Bwana kuandika orodha ya majina SASA HIVI. Hiyo ni kweli. Hata hivyo kuna Andiko linaloonesha kuandikwa katika siku zijazo. Ni katika Zaburi ya themanini na saba. Zaburi hii inazungumza habari za Bwana akiandika majina ya wale wote waliozaliwa katika Sayuni. Kabisa haiwezi kudhaniwa ya kwamba Mungu anapaswa kungojea hata mwisho wa nyakati ama kipindi hicho cha wakati kinachohusu Sayuni kusudi ajue ni akina nani wanaweza kuzaliwa Sayuni. Tena, hilo lingeondoa kule Kujua yote. Hakika Yeye anawajua wote wanaohusika katika hesabu hiyo. Lakini ni kitu gani? Je! si orodha tu iliyoandikwa upya ambapo Mungu anaweka tu katika orodha mpya yale majina yaliyosalia baada ya ufufuo wa pili nao walikuwa ni wa Sayuni? Hakika, hivyo ndivyo ilivyo.

*"Nami nitalikiri jina lake mbele za Baba Yangu, na mbele ya malaika Zake."*

Kuitwa majina mbinguni! "Mtu akifa, je! atakuwa hai tena? mimi ningengoja siku zote za vita vyangu, hata kufunguliwa kwangu kunifikilie. Wewe ungeita, nami ningekujibu; ungekuwa na tamaa ya kazi ya mikono Yako." Mchungaji Mkuu anawaita kondoo Wake kwa majina. Ile sauti ya Mungu ya uumbaji inawaita watoke mavumbini ama kubadilisha atomi zao hata ingawa hawakuwa wamelala. Ni kunyakuliwa. Ni ile Karamu kuu ya Ndoa ya Mwana-Kondoo na Bibi-arusi Wake.

Lakini kunyakuliwa sio kuitwa kwa majina pekee. Hapo kwenye ufufuo wa pili, kwenye ile hukumu ya kile Kiti kikuu Cheupe cha Enzi, majina yatakubaliwa mbele za Baba na malaika Zake. Sasa nimeambiwa na wale wanaojua, ya kwamba sauti iliyo tamu sana kwenye sikio la mwanadamu ni sauti ya jina la mtu huyo. Jinsi watu wanavyopenda kuwa majina yao mbele za watu. Jinsi wanavyopenda kusifiwa. Lakini hakuna sauti ya duniani itakayoweza kutaja jina lako kwa utamu kama sauti ya Mungu kama jina lako liko katika Kitabu cha Uzima na kubaki mle ili kufunuliwa mbele za malaika watakatifu. Hiyo itakuwa siku ya ajabu jinsi gani wakati tutakapomsikia Yesu akisema, "Baba, walikiri Jina Langu mbele za watu katika siku za safari yao duniani. Sasa nitayakiri majina yao mbele Zako na mbele za malaika wote wa mbinguni."

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Mara nyingine tena Roho amenena. Mara nyingine tena tumechunguza ushuhuda wa yale Roho aliyotuambia kwa wakati mwingine. Nasi tumeona kumbukumbu hiyo kuwa ni sahihi. Wakati mwingine umepita na umetimizwa kikamilifu kama Yeye alivyosema ungetimizwa. Ni faraja ya jinsi gani kwetu sisi tunaotarajia kuwa katika bibi-arusi wa siku ya mwisho, kwa kuwa inaifanya mioyo yetu iruke kwa furaha kwamba Yeye ni mwaminifu na atatimiza kila ahadi Yake. Kama Yeye alikuwa mwaminifu na wa kweli kwa wale wa Wakati wa Sardi, basi Yeye ni wa kweli vile vile tu kwa wakati wetu huu. Kama wao kwa neema Yake na nguvu Zake watapokelewa na kusifiwa Naye, basi na sisi pia. Hebu na tuendebasi, kwenye ukamilifu na kumlaki Bwana hewani, na tuwe pamoja Naye milele.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7